




MWONGOZO WA JIJI KUHUSU MAWIMBI YA JOTO KWA MATAWI YA **MSALABA MWEKUNDU NA HILALI NYEKUNDU**



MWONGOZO WA JIJI KUHUSU MAWIMBI YA JOTO

Kwa

Matawi ya Msalaba

Mwekundu na

Hilali Nyekundu

MWONGOZO WA JIJI KUHUSU MAWIMBI YA JOTO

Mawimbi ya joto ni hatari kwa maisha na athari zake zinazongezeka ulimwenguni kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo hili linaweza kuzuiwa; ni jukumu letu kuzuia changamoto hii ya afya ya umma isiathiri majirani, marafiki na hata familia zetu.

Kila mwaka, mawimbi ya joto husababisha vifo vya watoto wachanga, wazee na watu wenye matatizo ya kudumu ya kiafya. Kile kisichokubalika kuhusu dharura hii fiche ni kwamba hatua sahili, za gharama ya chini- kwa mfano wananchi wa kawaida kuwachunga majirani walio katika hatari ya kudhurika-zinaweza kuokoa maisha wakati wa matukio ya joto kali.

Takriban watu bilioni 5 wanaishi katika sehemu za ulimwengu ambapo mawimbi ya joto yanaweza kutabiriwa kabla hayajatukia, hii ina maana kwamba tuna muda wa kuchukua hatua za kuokoa maisha. Watu wanaoishi katika maeneo ya mijini wamo miongoni mwa wale wanaoathirika zaidi wakati mawimbi ya joto yanatukia kwa sababu maeneo haya yana joto zaidi na maeneo ya mashambani.

Zaidi ya nusu ya watu ulimwenguni wanaishi katika maeneo ya mijini na idadi hii inatabiriwa kuongezeka hadi theluthi mbili kufikia mwaka wa 2050. Ni muhimu kwa wafanyakazi wa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu pamoja nawatu wanaojitolea kufungamanisha hatua zao za kupunguza hatari za joto katika shughuli zao za kila siku katikia maeneo ya mijini.

Mwongozo huu unalenga kuwasaidia wafanyakazi na watu wanaojitolea katika matawi ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu kuelewa hatari za joto zinazowakabili, kushirikiana na wadau kujiandaa kuchukua hatua dhidi ya joto, na kufungamanisha hatua sahili, za gharama ya chini, zinazookoa maisha katika shughuli za kawaida za tawi. Mwongozo unaweza kutumiwa ukiwa pweke au pamoja na Mwongozo Kuhusu Wimbi la Joto kwa Majiji, ambao unawasaidia wafanyakazi wa jiji kuelewa hatari za joto, kubuni mfumo wa kutabiri dharura mapema na kurekebisha namna ya kupanga miji.

Wafanyakazi wa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu na watu waliojitolea kwenye mstari wa mbele wa dharura hii ya afya ya umma katika miji na majiji kote ulimwenguni, na kwa hivyo ni muhimu katika kuongoza juhudi za kuzuia vifo vinavyotokana na joto na vinaweza kuepukika.



Francesco Rocca
Rais wa IFRC

UTANGULIZI	8
KWA NINI MWONGOZO HUU?	8
NAMNA YA KUTUMIA MWONGOZO HUU	9
TUELEZE UNAYOFIKIRIA!	9
1. KUELEWA MAWIMBI YA JOTO	12
1.1 WIMBI LA JOTO NI NINI?	12
1.2 NANI YUMO KATIKA HATARI YA KUDHURIKA NA JOTO KALI?	14
1.3 WAPI KWENYE JOTO KALI ZAIDI?	16
1.4 NAMNA YA KUFUATILIA JOTO KALI	17
2. KUJIANDAAKWA AJILI YAWIMBI LA JOTO	18
2.1 NAMNA YA KUJUMUISHA JIJI LENU	18
2.2 KUSHIRIKIANA NA WADAU	19
2.3 UFADHILI KWA AJILI YA KUKABILIANA NA JOTO	19
2.4 KUJIANDAA KUKABILIANA NA JOTO	19
3. WAKATI WAWIMBI LA JOTO	20
3.1 UJUMBE KWA UMMA	20
3.2 ZIARA ZA NYUMBANI	21
3.3 ZIARA ZA SHULE	22
3.4 MAENEO YA KUSAMBAZA MAJI YA KUNYWA	23
3.5 MAENEO YA KUJITULIZA	24
3.6 HUDUMA YA KWANZA	25
3.7 USALAMA WA UFUONI NA WA MAJI	26
3.8 USALAMA MAHALI PA KAZI NA WA WAFANYAKAZI	27
3.9 USALAMA WA WATU WALIOJITOLEA	28
4. KUTATHMINI NA KUJIFUNZA BAADA YA WIMBI LA JOTO	30
5. KUJIANDAA KUKABILIANA NA WIMBI LA JOTOLINALOFUATA	31

ORODHA YA SHUGHULI	32
ORODHA YA UTENDAJI 1: Kueleza wimbi la joto	33
ORODHA YA UTENDAJI 2: Kuwapa wadau kipaumbele	34
ORODHA YA UTENDAJI 3: Kupanga ziara za nyumbani	35
ORODHA YA UTENDAJI 4: Kupanga ziara za shule	36
ORODHA YA UTENDAJI 5: Kutambua maeneo ya kusambaza maji ya kunywa	37
ORODHA YA UTENDAJI 6: Maeneo ya kujituliza	38
ORODHA YA UTENDAJI 7: Kutathmini hali baada ya wimbi la joto	39
KADI ZA HATUA	40
KADI ZA HATUA 1: Tangazo la vyombo vya habari	41
KADI ZA HATUA 2: Hoja kuu za kuangaziwa na vyombo vya habari	42
KADI ZA HATUA 3: Ziara za nyumbani	43
KADI ZA HATUA 4: Ziara za shule	44
KADI ZA HATUA 5: Brosha za ziara za shule	45
KADI ZA HATUA 6: Kutambua shinikizo la joto	46
KADI ZA HATUA 7: Kutoa huduma za kwanza kwa waliolemewa na joto	47
KADI ZA HATUA 8: Kutoa huduma za kwanza kwa walio na kiharusi	48
KADI ZA HATUA 9: Kuongea na wamiliki wa biashara	49
KADI ZA HATUA 10: Usalama wa wafanyakazi wakati wa joto kali zaidi	50
KADI ZA HATUA 11: Usalama wa watu waliojitolea	51
CHUNGUZI MAALUM	52
UCHUNGUZI MAALUM 1: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Kenya	53
UCHUNGUZI MAALUM 2: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam	54
UCHUNGUZI MAALUM 3: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa	55
UCHUNGUZI MAALUM 4: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi	56
UCHUNGUZI MAALUM 5: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India	57
UCHUNGUZI MAALUM 6: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina	58
UCHUNGUZI MAALUM 7: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Australia	59
UCHUNGUZI MAALUM 8: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania	60
UCHUNGUZI MAALUM 9: Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong	61
UCHUNGUZI MAALUM 10: Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan	62
UCHUNGUZI MAALUM 11 : Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam	63
UCHUNGUZI MAALUM 12: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania	64
KISANDUKU 1 : Ramani ya wimbi la joto	10
KISANDUKU 2: Kutambua watu walio katika hatari ya kudhurika	14
KISANDUKU 3: Kuwahimiza na kuwadumisha watu waliojitolea	29

Utangulizi



KWA NINI MWONGOZO HUU?

Mawimbi ya joto ni majanga hatari ambayo yanazidi kutukia na yanaweza kuathiri afya ya binadamu na ustawi wake kwa kiwango kikubwa. Wimbi la joto linapotokea, watu walio katika hatari ya kudhurika ndio wanaoathirika zaidi. Katika mwongo mmoja uliopita mawimbi makali ya joto yamechangia vifo vingi, ikiwemo vifo 400 nchini Uholanzi mnamo 2019, zaidi ya vifo 1,500 nchini India mnamo 2015, vifo 4,870 jijini Paris, Ufaransa manamo 2003, na zaidi ya vifo 10,000 nchini Urusi mnamo 2010. Takwimu hizi zaelekea ni makadirio ya chini kwa kuwa hakuna njia maalum ya kuhesabu vifo vinavyotokana na mawimbi ya joto Hivyo basi ni muhimu kwa Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu kufahamu hatari zinazotokana na mawimbi ya joto, kuelewa hatari ya kudhurika kwa makundi maalum na kuchukua hatua mahususi kuokoa maisha ya binadamu. Hata kama unaishi katika nchi ambapo kuna joto vipindi virefu mwakani, mahali ambapo joto halijawahi kuwa tatizo hapo awali, huenda likawa tatizo sasa kutokana na ongezeko la joto linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi. Hatua za dharura na kwa wakati za kupunguza wimbi la joto zinaweza kupunguza vifo vinavyotokana na joto kali kwa asilimia kubwa. Hatua hizi pia ni sahili, za gharama ya chini na zimo ndani ya mamlaka ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu.

Mwongozo huu umejikita kwa [Heatwave Guide for Cities](#)¹ lakini umeandaliwa mahususi kutoa hatua maalum ambazo zinaweza kutekelezwa na matawi ya Msalaba mwekundu na Hilali Nyekundu katika kujiandaa na kukabiliana na mawimbi ya joto katika miji na majiji. Licha ya kuwa baadhi ya hatua hizi ni ngeni, nyingi ya hatua zinazopendekezwa zinaweza kufungamanishwa na shughuli za matawi kwa urahisi.

Licha ya kuwa mawimbi ya joto yanaweza kuathiri maeneo ya mashambani na ya mijini, mwongozo huu umeandaliwa hususan kuangazia hatua katika maeneo ya mijini. Joto katika miji na majiji huelekeakuwa juu zaidi ya joto katika maeneo ya mashambani kutokana na hali nyingi- kama vile wingi wa

1 Singh, R., Arrighi, J., Jjemba, E., Strachan, K., Spires, M., Kadihasanoglu, A., [Heatwave Guide for Cities](#). 2019. Vituo vya Tabianchi vya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

majengo yaliyo karibu, barabara na njia-ambazo hunyonya joto na kuliachilia polepole. Hali hii hufanya miji na majiji kuwa joto zaidi kwa muda mrefu zaidi. Tawi lililoko katika maeneo ya mashambani linaweza kuamua kurekebisha baadhi ya hatua ili ziafiki vyema eneo hilo.

Tumeandika mwongozo huu kama kikundi, kwa kufanya mashauriano ya kina na wenzetu kutoka Mashirika ya kitaifa na IFRC. Tuna imani kuwa mwongozo huu ni rasilimali muhimu kwa wafanyakazi wa Shirika la Kitaifa na watu wanaojitolea kuwawezesha kuchukua hatua katika kujiandaa na kukabiliana na mawuimbi ya joto. Tunatambua mwitikio na maoni kuhusu mwongozo huu, au maelezo ya jinsi mapendekezo yametokelezwa. Tafadhali usisite kuyawasilisha kupitia barua pepe cities@climatecentre.org.

NAMNA YA KUTUMIA MWONGOZO HUU

Mwongozo umeundwa kuwa rahisi kutalii- kufuataramani sahili. Sehemu kuu ni *Kuelewa Mawimbi ya Joto*, ambapo tunatoa taarifa ya kimsingi kuhusu mawimbi ya joto, maeneo yaliyo katika hatari ya juu na makundi yaliyo katika hatari ya kudhurika; *Kujiandaa kwa ajili ya wimbi la joto* ambapo tunalenga ushirikiano na wadau wa jiji; *Wakati wa wimbi la joto* ambapo tunaeleza hatua za kuchukuliwa ili kusaidia kupunguza hatari za athari za joto miongoni mwa makundi mbalimbali yaliyo katika hatari ya kudhurika; na *Kutathmini na Mafunzo* ambapo tunatoa mwongozo wa jinsi ya kufanya tathmini ya baada ya hatua pamoja na kufungamanisha mafunzo katika *Kujiandaa kwa ajili ya wimbi la joto linalofuata* ambayo ni sehemu ya mwisho ya mwongozo huu.

Katika kile sehemu kuna orodha ya shughuli, kadi za hatua na uchunguzi maalum ambao unaweza kuwasaidia katika mchakato wenu wa kufanya mipango. Rasilimali hizi tofauti zimebainishwa kwa alama zifuatazo:



**UCHUNGUZI
MAALUM**



**ORODHA YA
SHUGHULI**



KADI ZA HATUA

TUELEZE UNAYOFIKIRIA!

Aghalabu tutatoa kitu kwa ulimwengu na hatupati kujua iwapo kilikuwa na manufaa au la na jinsi ya kukiimarisha.

Tafadhali tumia dakika 3 utupatie mwitikio kuhusu mwongozo huu kupitia: bit.ly/HWguideform

Tunapanga kutumia mwitikio huu kufanya marekebisho katika matoleo ya baadaye ya mwongozo huu, na kuunda rasilimali zaidi za kuwasaidia katika kazi yenu inayohusu mawimbi ya joto.

Ramani ya Maandalizi ili kukabiliana na Mawimbi ya joto



Kuelewa mawimbi ya joto


Wakati wa wimbi la joto



Kujiandaa kukabiliana na wimbi la joto






 Kujiandaa kukabiliana na wimbi la joto linalofuata



 Kufanya tathmini

1. Kuelewa mawimbi ya joto



1.1 WIMBI LA JOTO NI NINI?

Joto kali ni hatari kwa afya na ustawi wa binadamu, na hatari hii inaongezeka kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Tafiti nyingi zimeonyesha kuwa mabadiliko ya tabianchi tayari yamesababisha mawimbi ya joto makali, ya mara kwa mara na ya muda mrefu kuliko ilivyokuwa awali. Mtindo huu unatazamiwa kuendelea, na hata kuwa mbaya zaidi siku zijazo. Aina moja ya joto kali inaitwa “wimbi la joto.” Wimbi la joto aghalabu huwa ni janga linalosababisha vifo ambalo husababisha joto kali kuliko kawaida, au joto kali likiandamana na Unyevu mwingi, ambao huwa ni hatarikwa afya. Mawimbi ya joto kwa kawaida yna mwanzo na mwisho unaotambulika, hudumu kwa kipindi cha siku kadhaa na huathiri shughuli na afya ya binadamu. Hakuna ujelezi mmoja bia wa wimbi la joto kwa sababu viwango tofauti vya joto aghalabu huwa na athari tofauti katika maeneo tofauti ya dunia. Kwa mfano, jijini London, Uingereza, joto la nyuzi 28°C hudhukuriwa kuwa wimbi la joto, huku kwenye nyika za India, joto sharti lizidi nyuzi 40°C ili liweze kuitwa wimbi la joto. Joto jingi usiku linaweza kuwa kigezo muhimu cha kubaini wimbi la joto kwa sababu ni vigumu zaidi kwa mwili wa binadamu kupata nafuu kutokana na joto kali la mchana bila baridi ya usiku. Unyevu mwingi aidha hufanya vigumu kutokwa na jasho linalovukiza kutoka kwenye ngozi, njia mojawapo ya mwili wa binadamu kujituliza. Hivyo basi, joto na unyevu kwa pamoja ni muhimu katika kudhukuru hatari ya joto.

Kulinganisha ujelezi wa wimbi la joto

De Bilt,
Netherlands

New Delhi,
India

Cape Town,
Afrika Kusini

Ujelezi wa wimbi la joto

Angalau siku mbili mfululizo zenye joto linalozidi nyuzi 40°C kila siku

Angalau siku tatu mfululizo zenye joto linalozidi nyuzi 30°C kila siku

Angalau siku tano mfululizo zenye joto linalozidi nyuzi 25°C kila siku

Msimu wa joto

Aprili – Juni

Desemba – Februari

Juni – Agosti

Hatua zinazoweza kuchukuliwa

Njia maalum za kujituliza zinatumiwa, kama vile kulala ukiwa umejifunika kwa shuka baridi

Paa nyeupe zinaunwa kwa kuzipaka rangi, na hivyo zinarudisha miale ya jua na kupunguza joto katika majengo

Nyezo za kutuliza zinafunguliwa kote jijini ambapo watu wanaweza kutulia kwenye sehemu ya umma yenye kiyoyozi ili kuepuka joto

1. Kuelewa mawimbi ya joto



1.2 NANI YUMO KATIKA HATARI YA KUDHURIKA NA JOTO KALI?

Ni muhimu kujua kuwa yeyote anaweza kupata athari hasi kiafya au hata kufa kutokana joto kali. Hata hivyo, baadhi ya makundi ya watu aghalabu huwa katika hatari ya juu, ikiwemo watu wa umri wa juu, watoto wachanga, mama wajawazito na wanaonyonyesha, watu walio na matatizo ya kiafya, watu wa kipato cha chini, watu wanaofanya kazi nje au kupika ndani ya nyumba katika maeneo yenye majengo mengi kama vile mitaa ya mabanda na makaazi ya pamoja, na watu wasio na makao. Watu walio katika makundi haya huenda wakawa wazi kwa joto na/au miili yao huenda ikapata ugumu kudhibiti joto.

KISANDUKU 2: Kutambua watu walio katika hatari ya kudhurika

WATU WALIO KATIKA HATARI YA KUDHURIKA	VISABABISHI VYA HATARI
Watu wa umri wa juu (kama vile miaka 65 na zaidi)	Hawana uwezo mzuri wa kukabiliana na joto kali, wanaweza kuwa wametengwa kijamii, na huenda hawajui kuwa joto kali ni hatari. Watu wa umri wa juu pia huelekeo kutohisi kiu katika joto jingi, jambo ambalo huwatia katika hatari zaidi ya kudhurika kutokana na kupweka. Aidha, huenda wakawa wanatumia dawa ambazo hufanya vigumu kwao kudhibiti joto mwilini.
Watu walio na maradhi ya kuselelea.	Haya yanajumuisha ugonjwa wa moyo, mapafu na figo, kisukari na magonjwa ya akili. Dawa nyingi pia zinaweza kuongeza athari za joto kali.
Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano.	Ni wepesi kumia kutokana na athari za joto kali na sharti wawategemee watu wengine kuwatuliza na kuhakikisha wanapata maji ya kutosha.
Wanawake na wasichana	Kutegemea tamaduni na desturi za eneo, wanawake na wasichana huenda wakapata ugumu kufikia vyombo mbalimbali vya habari jambo ambalo hupunguza upataji wa tahadhari kuhusu wimbi la joto. Huenda wakalala katika vyumba ambavyo havipitishi hewa safi ipasavyo au wakakosa bafu zenye usiri hasa wakati wa hedhi, ambazo zinaweza kuwasaidia kujituliza.
Wanawake wajawazito na wanaonyonyesa	Wanawake wajawazito wanaelekea kupata maumivu ya kujifungua ya mapema katika juma linalofuata wimbi la joto. Hatari hii inazidi kadri siku zenye joto kali zinavyofululiza. Wanawake wanaonyonyesha wanahitaji kunwa maji mengi kwa kuwa kunyonyesha huchangia kupweka kwa njia kubwa.
Wafanyakazi wa nje(ikiwemo askari wa barabarani, walinzi, wachuuzi, wajenzi n.k.)	Aghalabu huhusika katika kazi zenye mavune wakati wakiwa wamemulikwa moja kwa moja na jua pamoja na joto na uchafuzi wa hewa. Wamo katika hatari ya kupweka na kupatikana na magonjwa ynayohusishwa na joto. Huenda wakahitajika kupunguza kiasi cha kazi ambayo wanafanya jambo linalopunguza kipato cha familia zao.
Wanariadha	Huhusika katika mazoezi makali ya kimwili, sanasana wakiwa nje, na yanaweza kuongeza joto mwilini kwa kazi na kusababisha kupoteza maji kupitia kwa kutokwa na jasho.

1. Kuelewa mawimbi ya joto

WATU WALIO KATIKA HATARI YA KUDHURIKA	VISABABISHI VYA HATARI
Watu waliotengwa au wanaoishi peke yao	Huenda wasipokee tahadhari wakati unaofaa au huenda wasiweze kufikia msaada kwa haraka.
Watu wanaoishi na ulemavu.	Huenda wasiweze kufikia maeneo ya kujituliza na huenda wasiweze kufikia msaada kwa haraka.
Watu walio na uzani wa juu na watu wanene sana	Huenda wakaathirika zaidi na joto kali na miili yao huenda ikapata ugumu kudhibiti joto mwilini.
Watu walio na kipato cha chini	Huenda wakakosa kufikia taarifa kuhusu mawimbi ya joto na/au vituo vya kujituliza pamoja na kuwa na rasilimali finyu. Huenda wasiweze kumudu kutokuwa kazini ili kuwatunza watu wa aila zao. Huenda wakahitajika kusafiri mwendo mrefu ili kufikia mahali pa kujituliza na huenda wakahisi kutotakikana katika sehemu fulani. Katika maeneo fulani huenda pia wakawa na ugumu kufikia maji safi ya kunywa.
Wahamiaji na wakimbizi	Huenda wasiweze kufikia taarifa za sasa za ushauri kuhusu joto na hatari za kiafya au huenda wakashuhudia hali za joto ambazo ni tofauti na za mahali walikotoka. Kaida hasi za kisheria au kitamaduni kwa wahamiaji na wakimbizi pia zinaweza kuchangia kuchelewa kwao kuwasiliana na watoaji wa huduma za dharura.
Watu wanaoishi katika maeneo yenye majengo mengi	Katika maeneo yenye majengo mengi-kama vile mitaa ya mabanda, bustani za kugesha makaazi na nyumba za ghorofa nyingi-familia nyingi hutumia eneo ndogo. Maeneo yenye majengo mengi yanaweza kuongeza athari ya kisiwa cha joto la mjini.
Watu wasio na makaazi	Huenda wasipokee tahadhari za mapema kwa wakati, huenda hawajui vituo vya kujituliza na huenda wasiweze kufikia njia nyingine za kujituliza (k.m bafu ya kujituliza). Huenda pia wakahisi kutokaribishwa kwenye vituo vya kujituliza kutokana na kutengwa na unyanyapaa.
Watu wenye kisomo cha chini na wasiosema lugha ya wenyeji	Hawawezi kusoma taarifa za sasa kuhusu tahadhari za joto na hatari za kiafya. Wasiosema lugha ya wenyeji huenda wasiweze kuelewa matangazo ya tahadhari kwenye runinga na redioni.
Watalii	Huenda wasiweze kuelewa tahadhari katika lugha za wenyeji. Huenda wasije namna ya kufikia vituo vya kujituliza, Bustani yenye miti au rasilimali nyingine, ikiwemo mifumo ya kusimamia dharura. Aidha, huenda wametoka maeneo yenye hewa baridi zaidi na hivyo wakashindwa kudhibiti joto.
Wanaohudhuria hafla	Huenda wakawa nje wakimulikwa na miale ya jua kali, au wakawa karibu na watu wengine bila kupata hewa safi, maji au mfumo wa baridi.
Makundi mengine yaliyotengwa kama vile LGBT, kutengwa kijiografia au makundi yaliyotengwa kitamaduni	Hutofautiana kutegemea kikundi ila pakubwa huhusishwa na unyanyapaa na kutengwa. Watu waliotengwa huhisi kuwa hawakaribishwa katika vituo vya kujituliza na huenda wakasita kuomba huduma za matibabu.
Wanyama/Mifugo/Wanyama vipenzi	Huwategemea wamiliki ili kulindwa kutokana na joto.

Imetoholewa kutoka kwenye maelezo ya Kansas Extreme Heat Toolkit²

2 Kansas Extreme Weather Workgroup (2014), Kansas Extreme Heat Toolkit, Topeka, Kansas. Imepakuliwa kutoka <http://bit.ly/2ZHE6oy>

1. Kuelewa mawimbi ya joto



1.3 WAPI KWENYE JOTO KALI ZAIDI?

Majengo katika jiji-saruji, lami na chuma- yanaweza kunyonya joto na kulinunurisha, na hivyo kufanya joto la jiji kuongezeka maradufu zaidi ya maeneo ya mashambani yaliyo karibu. Tukio hili huitwa athari ya kisiwa cha joto la mjini Katika baadi ya majiji, kunaweza kukawa na sehemu za jiji ambazo zina joto kali zaidi ya sehemu nyingine. Kwa mfano, katika Nairobi, Kenya mitaa ya mabanda mara kwa mara hupokea joto jingi kuliko maeneo mengine ya jiji kutokana na wingi na aina za majengo na kukosekana kwa bustani za miti. Hii inamaanisha watu wanaoishi katika maeneo haya wanapatwa na joto kali, na wanaweza kuwa katika hatari kubwa ya magonjwa yanayohusiana na joto. Wakati wa kushirikiana na serikali za mtaa kupanga harakati za kukabiliana na hali hizi, ni muhimu kuzingatia jinsi joto linaweza kutofautiana ndani ya jiji, ambapo joto ni kali zaidi, na mahali ambapo watu walio katika hatari ya kudhurika wanapatikana. Kuzingatia masuala haya husaidia kuelekeza harakati hizi ipasavyo. Kama makadirio ya jumla, maeneo yaliyo na bustani nyingi za miti huelekea kuwa matulivu zaidi. Ushirikiano na Chuo Kikuu katika eneo husika unaweza kuwa njia muhimu ya kutambua taarifa mahususi kuhusu jiji lenu.



UCHUNGUZI MAALUM 1: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Kenya

Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Kenya hushirikiana na wadau kutambua hatari zilizokithiri kutokana na joto katika mitaa ya mabanda jijini Nairobi.



UCHUNGUZI MAALUM 2: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam

Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Viet Nam, kwa msaada wa kiufundi kutoka kwa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Ujerumani, lilibuni mbinu za kubainisha athari likilenga kuchagua maeneo ya kutekeleza miradi katika Hanoi, Viet Nam.

1.4 NAMNA YA KUFUATILIA JOTO KALI

Katika maeneo mengi ya ulimwengu, hatari ya joto ni ya msimu-kuna kipindi cha mwaka kinachotarajiwa ambacho huwa na joto sana. Kwa mfano, nchini India kipindi hiki ni kuanzia Aprili hadi Juni kabla ya kuanza kwa msimu wa mvua, huku nchini Afrika Kusini kipindi hiki huwa ni wakati wa majira ya joto kuanzia Novemba hadi Februari. Mawimbi ya joto aghalabu yatatokea misimu hii; lakini pia yanaweza kutokea kwenye mipaka ya misimu hii. Ni muhimu kuelewa kuwa kuna “msimu wa joto” katika jiji lenu na msimu huu hutokea lini, ili muweze kulenga ufuatilizaji wenu katika miezi hiyo. Mawimbi ya joto ambayo hutokea kabla ya msimu huelekea kuwa hatari zaidi kwa sababu watu huwa hawajazoea vizuri joto linaloongezeka. Katika baadhi ya sehemu za ulimwengu, joto huwa sawa mwaka mzima; na, iwapo hii ndiyo hali, ni muhimu kuzidi kuchunguza utabiri wa hali ya hewa ili kutambu viwango vya juu vya joto visivyo vya kawaida kote mwakani. Idara yenu ya utabiri wa hali ya hewa huedna ikatoa taradhari za “joto kali” au “joto” katika vipindi hivyo. Iwapo hakuna, ni muhimu kuwasiliana na ofisi za idara ya utabiri wa hali ya hewa ili kutalii namna ya kubuni mfumo wa tahadhari kama huo. Mshirikiane na ofisi kuu za kitaifa za Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu pamoja na asasi za serikali zinazohusika, kama vile Idara ya Utabiri wa hali ya Hewa na Wizara wa Afya, ili kufuatilia joto kali, na kuhakikisha kwamba daima mnafamau utabiri wa hali ya hewa ya siku zijazo.



UCHUNGUZI MAALUM 3: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa

En collaboration avec les autorités locales, la Croix-Rouge française surveille les risques de chaleur pour les saisons, les semaines, voire les jours à venir, afin d'activer les mesures de sauvetage le cas échéant.



ORODHA YA UTENDAJI 1: Kueleza wimbi la joto

Orodha hii ya utendaji itawaelekeza kwenye maswali machache ya msingi ili kuelewa hali ya sasa ya taarifa kuhusu wimbi la joto katika jiji lenu.

2. Kujiandaa kwa ajili ya wimbi la joto



2.1 NAMNA YA KUJUMUISHA JIJI LENU

Jiji lenu huenda tayari lina Mpango wa Utendaji kuhusu Joto wakati wimbi la joto linapotokea nani anafanya nini kabla, wakati na baada ya wimbi la joto, pamoja na mikakati ya muda mrefu ya kupanga mji. Iwapo hati hii ipo, tafadhali isome (au uirejeele) Mpango huu huenda usiorodheshe moja kwa moja jukumu la Shirika la Msalaba Mwekundu au hilali Nyekundu, hivyo basi ni muhimu kuelewa na kueleza kile mnachoweza kutoa.

Iwapo hakuna mpango, Shirika la Msalaba mwekundu na Hilali Nyekundu linaweza kufanya kazi na wadau ili kuunda mpango. [Heatwave Guide for Cities](#), ulioundwa na Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu kwa ushirikiano na zaidi wa wenzi 25, ni rasilimali muhimu ambayo mnaweza kupendekeza kwa wenzenu kutoka kwa jiji lenu ili kuimarisha mpango wa utendaji kuhusu wimbi la joto.

Idara muhimu za jiji zinazoshughulikia joto zinajumuisha idara ya afya, idara ya utabiri wa hewa na idara ya huduma za dharura. Kushirikiana na idara ya upangaji kujumuisha mikakati ya kupunguza hatari za mawimbi ya joto katika mipango ya maendeleo ya jiji ni hatua inayopendelezwa pakubwa. Mwongozo kuhusu Mawimbi ya joto kwa Majiji pia ni rasilimali muhimu ya kushabikia mikakati ya muda mrefu ya kupunguza hatari kwa majiji.



ORODHA YA UTENDAJI 2: Kuwapa wadau kipaumbele

Orodha hii ya utendaji inatoa mwongozo wa kimsingi katika kutambua na kuwapa kipaumbele wadau wa kushirikiana nao ili kupunguza athari za joto.



UCHUNGUZI MAALUM 4: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi hushirikiana na wadau wa Mitaa na wa kitaifa kubuni mpango wa utendaji kukabiliana na joto nchini Uholanzi.

2.2 KUSHIRIKIANA NA WADAU

Mashirika yasiyo ya serikali yanatekeleza jukumu muhimu katika kujiandaa kukabiliana na mawimbi ya joto kwa sababu aghalabu haya tayari huwa yanashirikiana na watu walio hatarini ya kudhurika na yanaaminiwa na jamii. Ni muhimu kuwasiliana na viongozi wa Jiji na wadau wengine wa mashirika yasiyo ya serikali ili kuratibu shughuli hivi kwamba kila shirika litaangazia liliko na tajriba na uwezo na kuepuka ururdufishaji wa juhudi³. Wadau wa ziada wa kuhusisha ni kama vile vyombo vya habari, wahudumu wa afya, mashirika ya kidini, shule na waangalizi wa watoto, wenzi wa kibinafsi na wasomi.



2.3 UFADHILI KWA AJILI YA KUKABILIANA NA JOTO

Ili kujiandaa kukabiliana na wimbi la joto, ni muhimu kuelewa rasilimali mnazohitaji na vyanzo ambamo mnaweza kuzipata katika muktadha wa kitaifa na kieneo. Vyanzo vya ufadhili vinaweza kupatikana kupitia mipango ya kitaifa au ya baraza la miji inayolenga mabadiliko ya tabianchi na afya. Iwapo mnapanga kampeni kubwa huedna ikawa muhimu kuzingatia iwapo mtaomba msaada kutoka kwa mfidhili ambaye anafadhili miradi katika eneo lenu na ambaye anachangia miradi ya kujiweka tayari kwa mabadiliko ya tabianchi. Aidha, mnaweza kutumia fursa ili kubuni ushirikiano baina ya sekta ya umma na ile ya kibinafsi miongoni mwa makampuni yanayolenga kusaidia jamii katika jiji lenu. Katika hali hii, kampuni inaweza kutoa rasilimali kama vile michango au nafasi ya kuunda vituo vya kujituliza, au kutoa rasilimali kama vile maji au feni ambazo zinaweza kusambazwa kwa jamii.



2.4 KUJIANDAA KUKABILIANA NA JOTO

Kila shughuli iliyoorodheshwa katika sehemu inayofuata ya mwongozo huu inahitaji matayarisho ya namna fulani kabla ya wimbi la joto kutukia. Hii inajumuisha kutathmini mipango ya kukabiliana na wimbi la joto, kuandaa jumbe kwa manufaa ya umma kuhusu usalama kutokana na joto, kuwaelimisha watu waliojitolea, kuandaa ramani ya watu walio katika hatari ya kudhurika, kutambua maeneo ya kusambaza maji na kuandaa njia za kufuatwa wakati wa ziara za nyumbani. Kadri mnavyotathmini sehemu inayofuata, kwa kutumia mifano ya hatua ambazo zinaweza kuokoa maisha wakati wimbi la joto, kumbuka pia kutafakari juu ya matayarisho yanayohitajika ili kuchukua hatua kwa haraka. Matayarisho haya yanaweza kufanywa miezi kabla ya kuanza kwa msimu wa joto. Refelea orodha ya shughuli na kadi za hatua katika sehemu inayofuata kwa maelekezo ya kina zaidi kuhu jinsi ya kujiandaa.

3 Mamlaka ya umma wana jukumu la kutoa tahadhari. Kutegemea sheria za kitaifa, mashirika yasiyo ya serikali yanawza, au hayawezi, kuwa na mamlaka ya kutoa tahadhari.

3. Wakati wa wimbi la joto



Hatua za dharura na kwa wakati za kupunguza wimbi la joto zinaweza kupunguza vifo vinavyotokana na joto kali kwa asilimia kubwa. Hatua hizi pia ni sahili, za gharama ya chini na zimo ndani ya mamlaka ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu. Kuhakikisha kuwa watu wanadhibiti joto, wanakunywa maji ya kutosha na wanapokea huduma za matibabu kutaokoa maisha wakati wa wimbi la joto. Zifuatazo ni hatua za kimsingi za kuzuia vifo kutokana na wimbi la joto.



3.1 UJUMBE KWA UMMA

Wafanyakazi wa tawi na watu mashuhuri waliojitolea wanaweza kutekeleza jukumu muhimu katika kuhakikisha kwamba umma unatambua hatari inayowakabili wakati wa wimbi la joto na hatua gani wanaweza kuchukua ili kupunguza hatari za kimsingi⁴. Mahojiano na vyombo vya habari ni njia nzuri sana ya kuhakikisha ujumbe muhimu unafikia hadhira pana kadri inavyowezekana. Utabiri wa wimbi la joto unapotelewa, au pindi tu hapo baadaye, tawi linaweza kutoa tangazo kwa vyombo vya habari ili kufahamisha ishara za redio, runinga na hata magazeti kuwa wataalamu wa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu wapo tayari kutoa ushauri wa jinsi ya kuwa salama wakati wa wimbi la joto. Huduma za afya kwa umma za IFRC na vikasha vya huduma ya kwanza vinajumuisha mwongozo wa jinsi ya kuandaa ujumbe wa kubadili mienendo. Tawi linapaswa kutumia mitandao ya kijamii kama vile Twitter, Facebook, WhatsApp na TikTok kufikishia hadhira zaidi ujumbe wa kuokoa maisha. Kama hakuna utabiri uliotolewa, mawati yanaweza pia kupanga ujumbe wa mara kwa mara mwanzoni mwa msimu wa joto wakati ambapo hatari ya mawimbi ya joto iko juu.

4 Ujumbe kuhusu namna ya kuwa salama wakati wa wimbi la joto umo ndani ya mamlaka ya Mashirika mengi ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu. Hata hivyo, ni vyema kila mara kushirikiana na maafisa wa serikali, kama vile Wizara ya Afya, ili kuhakikisha ujumbe faafu, na sawa ndio unasambazwa.



KADI ZA HATUA 1: Tangazo la vyombo vya habari

Kadi hii ya hatua ni kiunzi cha kuandaa tangazo kwa vyombo vya habari kabla au wakati wa wimbi la joto. Likishakamilika, linaweza kupakiwa mtandaoni na kusambazwa kwa vyombo vingine vya habari.



KADI ZA HATUA 2: Points de discussion dans les médias

Kadi za hatua inatoa taarifa muhimu za kusambazwa kwa umma wakati wa mahojiano na vyombo vya habari.



UCHUNGUZI MAALUM 5: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India

Mbinu ngeni za shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India za kusambaza ujumbe kuhusu hatari za joto jijini New Delhi.



UCHUNGUZI MAALUM 6: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina hujenga ufahamu kuhusu hatari za joto kupitia kwa mitandao ya kijamii.

3.2 ZIARA ZA NYUMBANI

Miongoni mwa makundi yaliyo katika hatari ya kudhurika na joto ni watu walio na umri wa juu Wenye hali za kiafya za kuselelea, ambao wametengwa kijamii na wanaishi pweke. Watu katika kikundi hiki cha kidemografia mara kwa mara hupatikana na vifu vingi zaidi wakati wa wimbi la joto. Kutokana na haya, kila juhudi ya kuchunga usalama wao, kuhakikishawanakunywa maji na wanapokea huduma za matibabu inavyohitajika, itaokoa maisha. Mojawapo wa mkakati mzuri zaidi wa kufikia kikundi hiki cha kidemografia, makundi mengine yaliyokatika hatari ya kudhurika, ni kupitia ziara za nyumba hadi nyumba kutoka kwa watu wanaojitolea kwa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu. Nambari maalum ya simu ya kuwapigia simu wale waliokwisha sajiliwa awali ili kuwajulia hali pia ni muhimu. Watu waliojitolea wanaofanya ziara za nyumba hadi nyumba wanapaswa kupewa mafunzo ili kutambua dalili za ugonjwa unaotokana na joto na kutoa huduma ya kwanza inapohitajika.



ORODHA YA UTENDAJI 3: Kupanga ziara za nyumbani

Orodha hii ya Shughuli inatoa mwongozo wa kupatia kipaumbele mitaa na nyumba za kuzuru wakati wa kampeni dhidi ya wimbi la joto.



KADI ZA HATUA 3: Ziara za nyumbani

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo kuhusu kuendesha ziara za nyumbani na kutoa ujumbe wa kimsingi wakati wa ziara hizi.



UCHUNGUZI MAALUM 7: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Australia

Huduma ya Telecross REDi ambapo watu wanaojitolea kutoka kwa shirika la Msalaba Mwekundu nchini Australia huwapigia simu watu waliokwisha sajiliwa kila siku kuwajulia hali wakati wa mawimbi ya joto.



UCHUNGUZI MAALUM 8: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania

Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Uhispania hutoa taarifa muhimu kwa watu walio katika hatari kupitia kwa kampeni za ujumbe.

3. Wakati wa wimbi la joto



3.3 ZIARA ZA SHULE

Watu wanaojitolea kwa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu wanaweza kushirikiana na shule ili kuwasilisha ujumbe muhimu kuhusu usalama dhidi ya wimbi la joto kwa watoto. Isistoshe, zaidi ya kutoa taarifa ya msingi kwa wanafunzi kuhusu jinsi ya kuwa salama kutokana na wimbi la joto, kushirikiana na shule pia kunaweza saidia kuwasilisha ujumbe muhimu kuhusu hatari za joto kwa wazazi na familia. Kuwaomba wanafunzi wawaulize wazazi wao kuwajulia hali majirani wenye umri wa juu na watu aila yao kunaweza kuhakikisha kwamba, watu wa umri wa juu wanatunzwa wakati wa wimbi la joto. Shule zinazopatikana maeneo yenye majengo mengi sana jijini, ambapo athari ya kisiwa cha joto la mjini iko juu zaidi, zinapaswa kuwa miongoni mwa zile zinazopewa kipaumbele. Baadhi ya shule huenda zikahitaji mfumo wa kudhibiti joto kuhakikisha kwamba masomo yanaweza kuendelea kwa njia salama.



KADI ZA HATUA 4: Ziara za shule

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo wa kuendesha ziara za shule. Inatoa taarifa muhimu ya kusambazwa kwa wasimamizi wa shule pamoja na moja kwa moja kwa wanafunzi wakiwa darasani.



KADI ZA HATUA 5: Brosha za ziara za shule

Kadi za hatua ni brosha ambayo inaweza kuchapishwa na kusambazwa kwa wanafunzi.



ORODHA YA UTENDAJI 4: Kupanga ziara za nyumbani

Orodha hii ya Shughuli inatoa mwongozo wa kupatia kipaumbele shule za za kuzuru wakati wa kampeni dhidi ya wimbi la joto.



UCHUNGUZI MAALUM 9: Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong

Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong hutoa programu za mafunzo kwa shule ili kuimarisha ufahamu kuhusu hatari za joto na kupanua usambazaji wa taarifa kwa jamii pana zaidi.

3.4 MAENEO YA KUSAMBAZA MAJI YA KUNYWA



Maji yanaweza kusambazwa kwa umma pamoja na kuwekwa mahali mahususi ambapo watu walio katika hatari ya kudhurika huzuru mara nyingi. Kwa umma, usambazaji wa maji katika maeneo yenye shughuli nyingi ni mkakati mzuri ili kuwafikia watu wengi kadri inavyowezekana.

Dhukuru maeneo kama vile bustani za umma, sokoni, maeneo ya usafirishaji na maeneo yanayowavutia watalii. Zaidi ya umma kwa jumla, ni muhimu kuweka maeneo ya kusambaza maji ya kunywa mahali ambapo watu huzuru mara nyingi hasa wale walio katika hatari ya kudhurika na joto kali. Maeneo haya yanajumuisha maeneo ya ujenzi, vituo vya umma na mitaa ya watu wenye vipato vya chini. Tawi pia linaweza kushirikiana na asasi nyingine, kama vile maeneo ya ibada au ofisi za serikali za mitaa, ili kuhakikisha vituo vya maji ya kunywa vimesambazwa ipasavyo. Maeneo yote ya kusambaza maji yanapaswa kuandamana na ujumbe maalum wa kuwafahamisha watu namna ya kuwa salama wakati wa wimbi la joto. Mwisho, ni muhimu kutoa maji safi na salama ya kunywa, tukizingatia ubadhirifu. Kwa mfanio, mnaweza kuepuka kutumia chupa za maji za kutumiwa mara moja na badala yake mkatumia vifaa vinavyoweza kutumika tena.



ORODHA YA UTENDAJI 5: Kutambua maeneo ya kusambaza maji ya kunywa

Tumia orodha ya shughuli kutambua na kutoa kipaumbele kwa vituo vya kusambaza maji wakati wa wimbi la joto.



UCHUNGUZI MAALUM 10: Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan

Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan huwezesha maeneo ya kusambaza maji ya kunywa kulingana na utabiri.

3. Wakati wa wimbi la joto



3.5 MAENEO YA KUJITULIZA

Kujituliza, angalau kwa saa chache ndani ya siku, kunaweza kusaidia mwili wa binadamu kukabiliana na vipindi virefu vya joto. Wafanyakazi wa Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu wanapaswa kushirikiana na mamlaka za mitaa kuhakikisha kuwa wale walio katika hatari ya kudhurika na shinikizo la joto wanapata mahali pa kujituliza. Vituo vya umma, maktaba za umma na maeneo ya ibada, pamoja na maeneo mengine funge ya umma, yanaweza kuwa maeneo mazuri ya kuunda vituo vya kujituliza kwa kuhakikisha kuwa yamewekewa mifumo ya kufungulia na kufunga hewa baridi, pamoja na ilani zinazofaa na yako wazi kwa umma wakati wa mawimbi ya joto. (Tambua kuwa shule hazipaswi kutumiwa kama maeneo ya umma kukutana wakati wa masaa ya kusoma) Watu wanaojitolea kwa Msalaba mwekundu na Hilali Nyekundu wanaweza kusaidia kusimamia maeneo ya kujituliza na hivyo kuimarisha ufahamu wa eneo lao. Aidha, ni muhimu kuhakikisha kuwa maeneo ya kujituliza yako na maji kunywa na maji haya yamesambazwa kote jijini, ili kufikiwa kwa wepesi na kila mtu anayehitaji. Bustani za umma na maeneo mengine yenye miti yanaweza pia kutumiwa kama vituo vya kujituliza wakati wa mawimbi ya joto.



ORODHA YA UTENDAJI 6: Maeneo ya kujituliza

Orodha hii ya Shughuli inatoa mwongozo kuhusu mahali pa kuweka maeneo ya kujituliza na vituo vya kujituliza na jinsi vinaweza kufikiwa.



UCHUNGUZI MAALUM 11: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam

Wakati wa wimbi la joto mnamo Agosti 2019 Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam lilifungua vituo vya kutuliza joto na mabasi ya kutuliza joto ili kuwasaidia wakaazi wa Hanoi, nchini Viet nam kukabiliana na joto kali.

3.6 HUDUMA YA KWANZA

Huduma ya kwanza na huduma za matibabu ya dharura yanayofaa yanaweza kuokoa maisha wakati wa wimbi la joto. Ni muhimu kwa watu wanaojitolea walio na stadi za kutoa huduma ya kwanza wanaweza kutambua viwango tofauti vya shinikizo la joto, wanaweza kutoa huduma ya kwanza ya dharura kwa wagonjwa wanaohitaji na wanaweza kutoa rufaa kwa matibabu ya dharura kwa wale walio katika hali mbaya. Stadi hizi zikiwepo, wafanyakazi na watu wa kujitolea wanaweza kutoa msaada wa ziada kwa mamlaka ya mitaa wa wimbi la joto kwa kuwepo kwenye matukio ya michezo, mikutano ya hadhara na vituo vya kujituliza. Stadi zilizopo za huduma ya kwanza pamoja na nyenzo zinapaswa kutathminiwa na kuimarishwa ili kuakisi mwongozo bora zaidi uliopo kuhusu tiba ya wimbi la joto. Baadhi ya magonjwa yanayotokana na joto yanaweza kuchanganywa na hali nyingine na matibabu yasiyofaa yanaweza kusababisha vifo. Watu wanaojitolea ambao wameidhinishwa katika utoaji wa huduma ya kwanza lakini hawajapokea mafunzi maalum kuhusu tiba ya magonjwa yanayotokana na joto wanapaswa kupewa mafunzo ya ziada. Aidha, angalia App ya huduma ya kwanza ya IFRC ambayo inajumuisha mawimbi ya joto. Programu hii ya rununu inapatikana kwenye Google Play na kwenye Kasha la programu la Apple Huduma ya kwanza ya kimsingikwa magonjwa yanayohusiana na joto inaweza kujumuishwa katika mafunzo ya Kikosi cha Hatia cha Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu (RCAT).



KADI ZA HATUA 6: Kutambua shinikizo la joto

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kuhusu namna ya kutambua dalili za shinikizo la joto.



KADI ZA HATUA 7: Kutoa huduma za kwanza kwa waliolemewa na joto

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kuhusu namna ya kutambua dalili za shinikizo la joto.



KADI ZA HATUA 8: Kutoa huduma za kwanza kwa walio na kiharusi

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kuhusu huduma ya kwanza kwa walio na kiharusi.

3. Wakati wa wimbi la joto



3.7 USALAMA WA UFUONI NA WA MAJI

Ajali za kufa maji wakati wa joto kali huongezeka kwa kuwa watu huelekea ufuoni na maeneo mengine yenye maji- kama vile maziwa, mito na mabwawa — ili kujituliza. Watu waliojitolea wanaweza kuwekwa ili kutoa taarifa kuhusu usalama, vituo vya huduma ya kwanza na stadi za uopoaji kwenye maneno yenye maji. Wakati na baadaya wimbi la joto, matawi pia yanaweza kushirikiana na mamlaka ya mitaa kuongeza idadi ya maeneo salama yenye maji katika mipango ya mji, kama vile bustani za kunyunyiza na mabubujiko ambapo watu wanaweza kujituliza wakati wa joto kali.



UCHUNGUZI MAALUM 12 : Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania hufanya kazi ili kupunguza ajali za kufa maji wakati wa mawimbi ya joto.

3.8 USALAMA MAHALI PA KAZI NA WA WAFANYAKAZI



Maeneo ya kazi yanaweza kuzidisha athari za mawimbi ya joto, hasa wale walio katika majengo yasiyokuwa na mifumo ya kutosha ya kupitisha hewa safi au walio karibu na shughuli zinazozalisha joto la ziada. Watu wanaofanya kazi za sulubu nje wamo miongoni mwa makundi yaliyo katika hatari ya kudhurika na athari za mawimbi ya joto. Hii inaweza kujumuisha wafanyakazi wa viwanda, wafanyakazi wa mjengo, wanaofanya kazi za sulubu, askari wa barabarani na wanaotengeneza bustani. Shirika la Msalaba mwekundu na Hilali Nyekundu linaweza kushirikiana na waajiri ili kusaidia kuimarisha ufahamu wa hatari kubwa na kuwahimiza waajiri kutoa maji ya kunywa, kuongeza muda wa mapumziko na kuhakikisha kuna mfumo wa kutosha kupitisha hewa safi/ kusimamisha kazi kwa muda wakati joto ni kali sana ndani ya siku. Waajiri wanapaswa kuwahimiza wafanyakazi wao kuzingatia hatua za kinga zilizopo. Wafanyakazi na waajiri wanapaswa kupewa mafunzo ili kutambua dalili za shinikizo la joto na kutoa huduma za kwanza ya kimsingi.



KADI ZA HATUA 9: Kuongea na wamiliki wa biashara

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo na ujumbe muhimu kuhusu namna ya kusema na wamiliki wa biashara na meneja wa biashara kuhusu hatari za joto kali na usalama wa wafanyakazi.



KADI ZA HATUA 10: Usalama wa wafanyakazi wakati wa joto kali zaidi

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kwa wafanyakazi kuhusu jinsi wanaweza kuzuia shinikizo la joto mahali pa kazi. Inaweza kuchapishwa na kusambazwa wa wafanyakazi wengine na meneja. Toleo la bango la kadi hii pia linapatikana.

3. Wakati wa wimbi la joto



3.9 USALAMA WA WATU WALIOJITOLEA

Wakati wa wimbi la joto, ni muhimu kuhakikisha usalama wa watu waliojitoleakufanya ziara za nyumba hadi nyumba na kusimamia maeneo ya kusambaza maji inaweza ikawakazi ngumu wakati wa joto kali. Ni muhimu kuwakumbusha watu waliojitolea wahakikishe kuwa wanakunywa maji ya kutosha na kuwahitaji kupumzika mara kwa mara katika maeneo baridi ili kuhakikisha kwamba afya yao na usalama wao hauathiriki wanapowasaidia watu wengine. Nafasi za kujitolea zinapaswa kuwa na watu wa kutosha ili vipindi vya kujitolea viwe vifupi. Watu wowote waliojitolea na wanaonyesha dalili za shinikizo la joto wanapaswa kupewa huduma ya kwanza inayofaa au matibabu mara moja.



KADI ZA HATUA 11: Usalama wa watu waliojitolea

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo kwa watu waliojitolea kuhusu njia ya kuwa salama wakati wa shughuli za kuwafikia watu wakati wa mawimbi ya joto.

KISANDUKU 3: Kuwahimiza na kuwadumisha watu waliojitolea⁵

Juhudi za kupunguza athari za mawimbi ya joto zitategemea matendo ya watu waliojitolea. Kuhakikisha kuwa watu waliojitolea wamehamasishwa na kuzawadiwa kwa juhudi zao za kupunguza hatari za joto ni muhimu kwa mafanikio ya juhudi zote za matawi katika eneo husika.



Utambuzi wa watu waliojitolea ni njia mojawapo ya kuwahamasisha na kuwadumisha watu waliojitolea. Utambuzi unaweza kuwa wa njia tofauti tofauti. Unapaswa kutolewa kwa kuzingatia uhamasishaji wa watu waliojitolea na unapaswa kuwa umebinafsishwa, wa mara kwa mara na utolewe kwa watu wote waliojitolea. Baadhi ya mawazo yanayoweza kurekebisha ili kuafiki utamaduni wowote ni pamoja na:

- » kusema “asante” ya dhati
- » kufanya mpango kwao kupokea ujumbe uliobinafasishwa kutoka kwa msimamizi wao.
- » kujumuisha majina yao na picha katika machapisho au gazeti
- » kuwanunulia kahawa au chamcha
- » kukumbua tarehe yao ya kuzaliwa
- » kuwauliza maoni yao na kuwapana nafasi ya kushiriki katika maamuzi
- » kutathmini kazi yao kwa njia yenye maana na kwa kuwajali.
- » kubuni namna ya kujiendeleza kikazi ndani ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu
- » kuwapa nafasi ya kuibuka na mawazo bunifu
- » kutuma barua kutoka kwa bodi, meneja wa kitengo au ukurugenzi
- » kwapandisha cheo kwa kuwapa majukumu zaidi
- » kuwapa nafasi ya kushiriki utoaji wa mafunzo nje ya kitengo
- » kuwasifu mbele ya marafiki zao
- » tenga muda wa kusikiliza maoni yao
- » wajumuishe katika mikutano ya wafanyakazi
- » kulipa eneo au programu inayoenedelea jina lao
- » kuipa ,mbinu mpya, mchakato au mfumo jina la mtu wa kujitolea aliyeusanifu
- » kueleza shukurani kutoka kwa wateja, wanunuzi na wenzi
- » kutambua michango yao wakati wa sherehe kuu
- » kuwatuza cheti au kuwateua kupokezwa zawadi

5 Taarifa hii imetoholewa kutoka kwa ‘Usimamizi wa Watu waijojitolea katika jamii: Mwongozo wa Utoaji Mafunzo’ uliochapishwa na Muungano wa Kimataifa wa Shirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu mnamo 2009. Taarifa za kina zinapatikana kwenye kurasa za 39-41.

4. Kutathmini na kujifunza baada ya wimbi la joto



akati wa wimbi la joto, hatua aghalabu huhitaji kuchukuliwa dharura na hulenga utekelezaji. Baada ya kampeni dhidi ya wimbi la joto ni muhimu kutumia muda vyema ili kutafakari kama kikundi:

- » Tumeweza kutimiza nini?
- » Nini hakikutarajiwa?
- » Nini hakikuenda vizuri sana?
- » Nini kinaweza kufanywa tofauti wakati ujao?

Ni muhimu sana kutumia muda huu kutafakari kwa kuwa ni nafasi adimu ya kujifunza kutokana na tajriba, kuimarisha mipango ya kimkakati na, hatimaye, kushabikia utekelezaji wa shughuli kabla na wakati wa wimbi la joto. Aidha, ni muhimu kurekodi tafakari hizi za kikundi na kujumuisha mafunzo yaliyopatikana katika mipange ya baadaye.

Orodha ya shughuli 7 inatoa mwongozo wa jinsi ya kuendesha tathmini baada ya wimbi la joto. Wakati wa shughuli hii ni muhimu kukumbuka kuwa tathmini kama hii ya baada ya tukio inapaswa kufanywa punde tu baada ya wimbi la joto, wakati ambapo taarifa bado imo kwenye kumbukumbu za watu. Inapendekezwa kuwa na tathmini ya baada ya tukio ndani ya mwezi wa kwanza baada ya wimbi la joto kukamilika.

Ili kuimarisha hatua za kukabili wimbi la joto siku zijazo, ni muhimu kwa kila mtu kupata fursa y kueleza maohni yao na kila mtu kujua kwamba maoni yao yanakaribishwa. Wakati wa kubaini nini hakikuenda vizuri, washiriki wanapaswa kuhimizwa kutoa mapendekezo ya jinsi ya kuimarisha shughuli za baadaye. Wakati wa kueleza kile kilichoenda vizuri, ni muhimu kulenga ndipo ili utendaji mzuri utambuliwe na kurudufishwa. Ni muhimu kwa washiriki wote kufanywa kuhisi kwamba wana sauti sawa na kwamba maoni yao yanathaminiwa, ahata kama yanatofautiana na yale wa wafanyakazao au watu waliojitolea wa kiwango cha juu.



ORODHA YA UTENDAJI 7: Kutathmini hali baada ya wimbi la joto

Mwongozo wa jinsi ya kutekeleza tathmini ya ndani kwa ndani baada ya shughuli na kurekodi mafunzo yaliyopatikana baada ya wimbi la joto.

5. Kujiandaa Kukabiliana na wimbi la joto linalofuata

Muda wa punde tu baada ya wimbi la joto ni wakati mzuri pia wa kuimarisha msukumo wa kampeni i ayofuata dhidi ya wimbi la joto kwa kushirikiana kwa karibu na wenzi maalum- kama vile halmashauri ya mitaa, vyuo vikuu, bishara, mashirika yasiyokuwa ya serikali, mashirika ya kidini n.k.- ili kuimarisha uratibu wa mipango ya kampeni dhidi ya wimbi la joto linalofuata, huku mafunzo yakidokezwa kutokana na hatua dhidi ya wimbi la joto lililokamilika.

Hiki ni kipindi kizuri cha kulenga kimkakati uchangishaji wa pesa za kutumiwa katika kampeni dhidi ya wimbi la joto linalofuata, ili kuwa tayari kuchukua hatua faafu pindi tu wimbi la joto linapotangazwa. Aidha, ni muhimu kujumuisha mawimbi ya joto kwenye mipango ya kukabiliana na majanga ya Mashirika ya Kitaifa na Matawi. Isitoshe, matawi yanaweza kurekebisha nyenzo zilizopo kama vile tathmini za kuwa katika hatari ya kudhurika na uwezo ili kujumuisha mawimbi ya joto.

Aidha, ili kujiandaa kwa kampeni inayofuata, matawi ya Msalaba mwekundu yanapaswa kushirikiana na maafisa wa jiji kuhakikisha mipango ya mji ya muda mrefu inapunguza makali ya joto kali siku za usoni pamoja na kupunguza athari za mawimbi ya joto. Wafanyakazi wa tawi wanaweza kutekeleza dhima muhimu katika kuhamasisha watetezi katika jamii na kushirikiana na mamlaka ya serikali za mtaa ili kukubali mipango bora ya upangaji wa mji ili kupunguza joto kwa ujumla katika jiji.

Hatua za kupewa kipaumbele zinajumuisha kulinda na kuongeza bustani zenye miti kote jijini, kuongeza ufikiaji wa vituo vya maji kwa umma, kukarabati majengo kwa kuweza paa zinazorudisha joto na mikakati ya kiasili ya kutuliza hewa pamoja na kushirikiana na mifumo ya afya kujiandaa kwa dharura za baadaye. Mapendekezo haya yameelezwa katika [Heatwave Guide for Cities](#)⁶. Ni sehemu nzuri ya kuanzia katika kusambaza rasilimali hii kwa wenzenu kutoka serikali za mitaa katika kujadili mikakati ya muda mrefu ya kupunguza hatari za mawimbi ya joto.

6 Singh, R., Arrighi, J., Jjemba, E., Strachan, K., Spires, M., Kadhihasanoglu, A., [Heatwave Guide for Cities](#). 2019. Red Cross Red Crescent Climate Centre

Orodha ya shughuli



ORODHA YA UTENDAJI 1: Kueleza wimbi la joto

Orodha hii ya utendaji itawaelekeza kwenye maswali machache ya msingi ili kuelewa hali ya sasa ya taarifa kuhusu wimbi la joto katika jiji lenu.

KUHUSU JIJI LENU

Je, kuna “msimu wa joto” katika jiji lenu ambapo joto huelekea kuwa kali zaidi?

Iwapo ndito, hali hii hutokea lini mwakani? (k.m. Aprili-Mei) _____

Ni kiwango gani cha joto hudhukuriwa kuwa kali, au hatari katika jiji lenu? _____

Je, jiji lenu lina unyevu? _____

Je, kuna utabiri wa mawimbi ya joto unaotolewa na idara za utabiri wa hali ya hewa?

Iwapo ndiyo, unaufikiaje? _____

Je, kwa kawaida utabiri huu hutolewa siku ngapi kabla ya wimbi la joto? _____

Nani matu wa kuwasiliana naye katika idara ya utabiri wa hali ya hewa? _____

Je, jiji lenu lina Mpango wa Kukabiliana na Wimbi la Joto?

Iwapo ndiyo, ni idara gani za serikali zinahusika? _____

Nani matu wa kuwasiliana naye katika mamlaka ya jiji? _____

Je, mna nakala ya mpango huo? _____

Uwezo wenu na ufahamu wenu ni upi?

Je, Shirika lenu la Kitaifa lina ufahamu kuhusu hatari zinazohusiana na mawimbi ya joto? _____

Je, Shirika lenu la Kitaifa linajua Hatua za kuokoa maisha ambazo linaweza kutekeleza? _____

Je, Shirika lenu la Kitaifa lina utaratibu wa huduma ya kwanza Uliorekebishwa kuafiki mawimbi ya joto? _____

Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu inaweza kusaidia vipi?

Nini huduma za kimsingi zinazotolewa na Shirika lenu la Kitaifa? _____

Je, shughuli za kujiandaa kwa ajili ya wimbi la joto, hatua za mapema na kukabiliana na wimbi la joto zinaweza kujumuishwa katika huduma hizi?

Iwapo ndiyo sitajumuishwa vipi? _____

Mnahitaji rasilimali gani ili kufanya hivi? _____

Orodha hii ya shughuli itawasaidia kitathmini taarifa, uwezo na nafasi ambazo Shirika lenu la kitaifa linapaswa Kushughulikia kukabiliana na wimbi la joto. Itawasaidia kuelewa ni maeneo gani ambayo huenda yakahitaji kuangaziwa zaidi Mnapoanza kushughulikia Mawimbi ya joto.

Orodha ya shughuli



ORODHA YA UTENDAJI 2: Kuwapa wadau kipaumbele

Orodha hii ya shughuli inatoa mwongozo wa kimsingi katika kutambua na kuwapa kipaumbele wadau wa kushirikiana nao ili kupunguza athari za joto.

Mamlaka ya kupunguza hatari zinazotokana na joto hayamo chini ya Taasisi moja, sekta au idara ya jiji. Badala yake, kuna Wadau tofauti ambao wana majukumu muhimu ya kutekeleza katika juhudi nzima za kupunguza athari za joto kali. Kuanzisha au kuimarisha ushirikiano na wahusika hawa kutasaidia kuhakikisha kukabiliana na matukio ya joto kali kwa njia faafu, huku kukitoa nafasi za kuibuka na mikakati ya muda mrefu ya kupunguza joto. Tumia nafasi Kutambua wadau muhimu wa kushirikiana nao kwa kutumia orodha hii.

Idara ya kitaifa ya utabiri wa hali ya hewa au mashirika mengine yanayosimamia utoaji wa ilani kuhusu wimbi la joto:

»

»

»

Maeneo ya mtagusano na serikali za mitaa katika upangaji wa mji, kukabiliana na dharura na husuma za kijamii:

»

»

»

Vituo vya kijamii, makundi ya kidini na makundi mengine yasiyokuwa ya serikali ambayo hutoa huduma kwa watu wa umri wa juu na makundi mengine yaliyo katika hatari ya kudhurika:

»

»

»

Wanahabari wa kusaidia kusambaza taarifa kuhusu hatua za kupunguza hatari inayotokana na joto:

»

»

»

Wenzi(serikali, sekta ya umma na ya kibinafsi)walio na wafanyakazi ambao wanafanya kazi nje au katika maeneo yasiyokuwa na mfumo tosha wa hewa safi:

»

»

»

Taasisi za elimu/idara zinazotafitia joto kali jijini:

»

»

»

Taasisi za afya (hospitali, kliniki kuu, maeneo ya kutunza wa wakongwe n.k.):

»

»

»

Tanbihi: shule pia ni wenzi muhimu Orodha ya shughuli 4 inatoa taarifa za kina zaidi kuhusu shule.



ORODHA YA UTENDAJI 3: Kupanga ziara za nyumbani

Orodha hii ya Shughuli inatoa mwongozo wa kupatia kipaumbele mitaa na nyumba za kuzuru wakati wa kampeni dhidi ya wimbi la joto.

Mitaa gani katika jiji lenu inaelekea kuwa wa watu wa umri wa juu wengi zaidi ya mitaa mingine?

»
»
»

Mitaa gani katika jiji lenu ni ya watu wa kipato cha chini?

»
»
»

Mitaa gani ya makaazi katika jiji lenu hupata joto kali zaidi? (Sana sana mitaa ina bustani chache zenye miti na imejengwa kwa nyenzo zinazonyonya joto.)

»
»
»

Je, kuna mitaa ambamo wahamiaji wengi wageni hupendelea kuishi? Iwapo ndiyo, ni ipi?

»
»
»

Mnahitaji rasilimali gani ili kufanya hivi?

»
»
»

Kwa pamoja, mitaa hii ndio mahali pazuri pa kupewa kipaumbele katika ziara za nyumba hadi nyumba, hasa mitaa inayotokea katoka orodha mbili au zaidi. Isitoshe, vifuatavyo ni vidokeza zaidi:

1. Shirikiana na asasi zinazohudumu katika mitaa iliyobainishwa ili kuwa na athari kubwa zaidi. Tazama *Orodha ya Shughuli 2* kwa mawazo kuhusu asasi za kushirikiana nazo. Jiji lako huenda lina ofisi ya wakongwe ambayo inaweza kutoa ushauri kuhusu njia nyingine ya kufikia watu wa umri wa juu.
2. Waalike watu kujisajili kabla, au wakati wa wimbi la joto, kwa ziara za watu wa kujitolea. Hili linaweza kufanywa kupitia njia ya simu au kwa kutembelea vituo vya umma na maeneo mengine ambapo watu wa umri wa juu huzuru mara kwa mara.
3. Wasiliana na vyuo vikuu jijini kubaini iwapo vimefanya utafiti faafu wa eneo la mji ambao umebainisha kwa uwazi zaidi mitaa na makaazi yaliyo katika hatari.

Wakati wa kampeni dhidi ya wimbi la joto, kuwafikia watu walio katika hatari ya kudhurika na mawimbi ya joto ni shughuli mojawapo faafu mnayoweza kufanya. Oroska hii inatoa mwongozo wa kimsingi kuhusu jinsi ya kutambua na kutoa kipaumbele kwa makaazi yaliyo katika hatari ya kudhurika kipitia kwa mtazamo wa mitaa. Baada ya kutoa kipaumbele kwa mitaa ya kuzuru, mnaweza sasa kufuata mwongozo uliopo kama vile mwongozo wa Afya ya jamii na Huduma ya kwanza⁷ kuhusu namna ya kuendesha ziara za nyumbani.

7 International Federation of Red Cross Red Crescent Societies (IFRC), Community-based Health and First Aid. 2009, IFRC Geneva, Switzerland



ORODHA YA UTENDAJI 5: Kutambua maeneo ya kusambaza maji ya kunywa

Tumia orodha ya shughuli kutambua na kutoa kipaumbele kwa vituo vya kusambaza maji wakati wa kampeni dhidi ya wimbi la joto.

Ili kufikia umma, maeneo yafuatayo yamepewa kipaumbele

Maeneo ya usafiri:

»
»

Bustani za umma, soko na mahali pengine pa hadhara:

»
»

Maeneo ya kuwavutia watalii au maeneo mengine yenye hafla:

»
»

Ili kufikia watu walio katika hatari kubwa ya kudhurika, maeneo yafuatayo yamepewa kipaumbele

Maeneo ya ujenzi:

»
»

Mitaa ya watu wa kipato cha chini (zingatia ofisi za serikali na maeneo ya ibada ili maji ya kunywa yasambazwe ipasavyo):

»
»

Sasa Chunguza:

1. Je, kuna mitaa yoyote ambayo haipo? Je, kuna wingi wa maeneo katika mtaa wowote?
2. Je, mitaa ya watu wa kipato cha chini imeangaziwa ipasavyo?
3. Je, kuna watu wa kujitolea wa kutosha kusimamia maeneo yote huku mkihakikisha zamu fupi za kazi ili kulinda usalama na afya yao?

VIDOKEZO

- Jadilianeni na jamii zinazohusika mnapoamua vituo vya kusambaza maji. Kwa mfano, kituo kilichotambuliwa kwenye ramani huedna kikaonekana kuwa faafu lakini huedna hakiwezi kufikiwa kwa wepesi kwa kutumia usafiri wa umma.
- Fanyeni mpango wa jinsi watu walio katika hatari ya kudhurika katika jamii, ambao huenda hawawezi kutoka nyumbani kwao au hawawezi kufikia vituo vya usambazaji, bado wanaweza kupokea msaada na maji.
- Mnapoteua vituo vya kusambaza maji ya kunywa, hakikihsa kwamba kuna kivuli ndipo watu wasilazimike kusubiri foleni chini ya jua kali.
- Jaribuni kutafuta vifaa safi na salama badala ya kutumia vikombe na chupa za plastiki zinazotupika. Wakati vikombe vya kutupika sharti vitumike, heri kutumia kombe vya karatasi badala ya vya plastiki na stairofomu.
- Hata hivyo, katika baadhi hali- kama vile kiangazi kikali na joto kutokea pamoja- chupa za maji huenda zikawa chaguo bora zaidi.



ORODHA YA UTENDAJI 6: Maeneo ya kujituliza

Orodha hii ya Shughuli inatoa mwongozo kuhusu mahali pa kuweka maeneo ya kujituliza na vituo vya kujituliza na jinsi vinaweza kufikiwa.

Kituo cha kujituliza ni Mahali katika jamii ambapo watu wanaweza kujituliza wakati wa joto kali, hasa pale ambapo hawana viyoyozi. Kwa kawaida, maeneo ya kujituliza huwa na kiyoyozi na yanafikiwa na watu wote jijini bila kizuizi. Iwapo maeneo ya kujituliza yenye viyoyozi hayapatikani, basi maeneo ya nje ya mapumziko- kama vile bustani, mabwawa/ bustani za kunyunyiza na ufuo wenye huduma za uopoaji, maziwa na vidimbwi vya umma vya kuogelea — Pia ni maeneo ya Kutuliza joto. Vituo vya muda vinaweza kuundwa katika hema zenye feni na kiyoyozi. Hema hizi zinapaswa kufikia umeme na maji , na ziwekwe kwenye kivuli (k.m. chini ya mti). Isitoshe, hakikisha kwamba watu wanaosimamia vituo vya kutuliza joto wamepewa mafunzo ya huduma ya kwanza kwa magonjwa yanayohusiana na joto.

Où est-il possible d'installer des centres de rafraîchissement dans votre ville ? Ni maeneo gani yanayoweza kutumiwa kuweka vituo vya kutuliza joto katika jiji lenu? Kumbuka, vituo vya kujituliza vinajumuisha maeneo ya ndani yaliyo na kiyoyozi kama vile maktaba, vituo vya jamii na vya wakongwe, vyuo vikuu na majengo ya jumla.

»

»

»

Vituo vya kutuliza joto hutoa nafasi kwa ushirikiano baina ya sekta ya umma na ile ya kibinfasi. Je, kuna kampuni za kibinafsi katika jiji lenu ambazo huenda zikawa radhi kuruhusu Msalaba Mwekundu au Hilali Nyekundu kutumia maeneo yao yaliyo na viyoyozi wakati wa wimbi la joto? Andaa orodha ya wenzi wote wanaowezezana:

»

»

»

Iwapo viyoyozi havipo, je, juna maeneo mengine ya kujituliza ambayo wakaazi wa jiji wanaweza kutumia kujituliza kutokana na joto? Andaa orodha ya maeneo hayo:

»

»

»

Je, kuna njia za kuunda maeneo ya muda ya kujituliza?

Kwa mfano, kuweka bustani ya kunyunyiza au kuongeza kivuli katika maeneo fulani ya umma? Orodhesha mawazo yako:

»

»

»

Je, watu watafikaje kwenye maeneo ya kujituliza? Inaweza ikawa kwamba huduma ya kuwapeleka na kuwarejesha watu inahitajika wakati wa wimbi la joto, hasa iwapo kuna maeneo machache ya vituo vya umma vya kutuliza joto na hiviwezi kufikiwa kwa urahisi. Orodhesha mawazo yako ya kutoa usafiri:

»

»

»



ORODHA YA UTENDAJI 7: Kutathmini hali baada ya wimbi la joto

Mwongozo wa jinsi ya kutekeleza tathmini ya ndani kwa ndani baada ya shughuli na kurekodi mafunzo yaliyopatikana baada ya wimbi la joto.

Awamu ya kwanza ya tafakari:

Nini kilienda shwari?

- »
- »
- »
- »
- »

Awamu ya pili ya tafakari:

Nini kilikuwa kigumu? Nini hakikuenda vizuri sana?

- »
- »
- »
- »
- »
- »

Awamu ya tatu ya tafakari:

Nini kinaweza kufanywa tofauti wakati ujao?

- »
- »
- »
- »
- »

Baada ya kuchukua hatua kadhaa dhidi ya wimbi la joto, ni muhimu kukusanya kikosi na kutafakari nini kilichoweza kutimizwa, changamoto zipi zimeshuhudiwa na nini kifanywe tofauti wakati ujao. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha kuwa mipango ya kimakakati — Inaweza kuimarishwa kwa kuzingatia mafunzo muhimu.

Kadi za hatua



KADI ZA HATUA 1: Tangazo la vyombo vya habari

Kadi hii ya hatua inaweza kutumiwa kama mwongozo wakati wa kuibuka na tangazo kwa vyombo vya habari kabla au wakati wa wimbi la joto kwa kubadilisha matini yote yaliyo kwenye [mabano] kwa ujumbe mahususi kwa tukio. Likishakamilika, linaweza kupakiwa mtandaoni na kusambazwa kwa vyombo vya habari.

TANGAZO LA VYOMBO VYA HABARI [WEKA JINA] WIMBI LA JOTO - WATAALAMU WA MSALABA MWEKUNDU WAPO

[Mahali], [Tarehe ya kutolewa] - **Wataalamu wa Msalaba Mwekundu wapo tayari kujadili athari zinazoweza kwa masilahi ya binadamu kutokana na wimbi la joto la juma hili kule [jina la mahali] pamoja na hatua sahili na za gharama ya chini zinazoweza kuhukuliwaili kulinda maisha.**

Viwango vya joto vinatarajiwa kupanda juu katika kipindi cha siku kadhaa zijazo, na hivyo kuweka shinikizo kwa mifumo ya afya na masilahi ya kijamii, na hata kuhatarisha maisha na usalama wa watu walio katika hatari ya kudhurika.

Wataalamu wa Msalaba Mwekundu wanaweza kudokeza baadhi ya hatua kamili, za kuokoa maisha ambazo watu na mamlaka yanaweza kuchukua ili kupunguza athari kwa masilahi ya binadamu inayotokana na wimbi la joto.

Wataalamu wanaopatikana ni pamoja na:

Katika [mahali]: [jina], [cheo], [uwanja maalum wa utaalumu inapohitajika]

Katika [mahali]: [jina], [cheo], [uwanja maalum wa utaalumu inapohitajika]

Mwanahabari:

Katika [mahali]: [jina], [cheo], [nambari ya simu], [barua pepe]



KADI ZA HATUA 2: Hoja kuu za kuangaziwa na vyombo vya habari

Kadi hii ya hatua inaweza kutumiwa kama mwongozo wakati wa kuibuka na tangazo kwa vyombo vya habari kabla au wakati wa wimbi la joto kwa kubadilisha matini yote yaliyo kwenye [mabano] kwa ujumbe mahususi kwa tukio. Likishakamilika, linaweza kupakiwa mtandaoni na kusambazwa kwa vyombo vya habari.

Ujumbe muhimu 1:

Mwimbi ya joto husababisha vifo, lakini vifo vinavyotokana na joto vinaweza kuzuiwa kwa hatua sahili za gharama ya chini.

- Ingawa mawimbi ya joto hayana athari sawa inayoonekana kama ilivyo kwa majanga kama vile mafuriko na kibunga, yangali miongoni mwa majanga asilia ambayo ni hatari sana yanapotokea.
- Walio walio katika hatari kuu ya kuathirika na joto ni watoto wachanga na watu wa umri wa juu, watu wenye maradhi ya kuselelea (kama vile ugonjwa wa moyo, ugonjwa wa mapafu, kisukari na magonjwa ya akili), watu wanaofanya kazi nje na watu waliotengwa.

Ujumbe muhimu 2:

Kunywa maji ya kutosha kunaweza kupunguza athari za joto kali.

- Njia mojawapo ya kukabiliana na joto ni kunywa maji ya kutosha kabla hujahisi kiu.
- Wakati wa joto kali, unapaswa kuepuka kunywa kinywaji chenye kafeini na vileo.

Ujumbe muhimu 3:

Kujituliza, angalau kwa saa chache ndani ya siku, kunaweza kusaidia mwili wa binadamu kukabiliana na joto kali.

- Haya ni maeneo jijini ambamo mtu anaweza enda kujituliza: [Weka jina la maeneo mahususi jijini kama vile maeneo yenye viyoyozzi, bustani za umma, maeneo yenye maji na huduma za uopoaji, bustani za kunyunyiza n.k.]
- Iwapo unaelekea kwenye [ufuo, ziwa n.k.] au kwenye vituo vingine vilivyo na maji, kumbukan kuzingatia usalama majini. Ajali za kufa maji huongezeka wakati wa mawimbi ya joto.

Ujumbe muhimu 4:

Wajulie hali jamaa, marafiki na majirani. Iwapo wewe au wapendwa wako wataanza kuonyesha dalili za shinikizo la joto kali, jitulize haraka na utafute huduma za matibabu.

- Dalili za shinikizo la joto kali zinajumuisha kutapika, kukanganyikiwa, kutojifahamu, ngozi moto iliyokauka na kupotewa na ufahamu.

VIDOKEZO

- Mahojaiano na vyombo vya harabi aghalabu huwa mafupi, kuwa tayari kutoa taarifa muhimu katika muda wa dakika mbili au tatu. Muulize mwanahabari utapewa dakika ngapi ili uweze kujiandaa.
- Taarifa zilizo katika rangi iliyokolezwa ndizo muhimu zaidi, hakikisha umezisambaza zote kwa muda uliotengewa.
- Chunguza kuhakikisha kwamba Shirika la kitaifa lina msemaji aliye na uelewa afanye mahojiano na vyombo vya habari.



KADI ZA HATUA 3: Ziara za nyumbani

Kadi hii ya hatua inatoa ujumbe muhimu kwa watu waliojitolea kusambaza wakati wa ziara za nyumbani. Ichapishe na uibebe.

Ujumbe muhimu:

- Eneo hili kwa sasa linashuhudia joto kali.
- Joto linaweza kuwa hatari kwako na kwa familia yako, hasa kwa watu wa umri wa juu, watoto wachanga, mama wajawazito na wale wanaougua kisukari, ugonjwa wa moyo au matatizo ya kupumua.
- Wewe na familia yako mnaweza kuwa salama kwa kunywa maji ya kutosha, kunywa maji kabla ya kuhisi kiu na kuepuka kunywa vinywaji vilivyo na kafeini au vileo.
- Wewe na familia yako mnaweza kuwa salama kwa kuzuru maeneo ya kujituliza ili kupunguza makali ya joto. Eneo la kujituliza lililo karika nawe ni [WEKA ENEO].
- Unaweza kuwasaidia marafiki na jamaa kuwa salama kwa kusambaza ujumbe huu na mara kwa mara kuwajulia hali wale walio katika hatari ya kudhurika.
- Iwapo wewe au mtu unayemjua ataanza kuonyesha dalili za ugonjwa unaohusishwa na joto, Dalili za shinikizo la joto kali zinajumuisha kutapika, kukanganyikiwa, kutojifahamu, ngozi moto iliyokauka na kupotewa na ufahamu.
- Dhibiti joto nyumbani kwa:
 - a.** Kuhakikisha hewa safi inaingia jioni iwapo nje kuna hewa tulivu kuliko ndani.
 - b.** Kufunika madirisha mchana, ili kuzuia jua, iwapo kuna joto kali nje kuliko ndani.
 - c.** Epuka kupikia ndani ya nyumba, na badala yake kula chakula baridi. Iwapo unahitaji kupikia ndani ya nyumba, funika surufia ili kupunguza unyevu ndani ya nyumba.

Tanbihi :

Ifuatayo ni mifano ya taarifa muhimu ambayo inapaswa kuwekwa katika muktadha kwa ushirikiano na Wizara yenu ya Afya.



KADI ZA HATUA 4: Ziara za shule

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo wa kuendesha ziara za shule. Inatoa taarifa muhimu ya kusambazwa kwa wasimamizi wa shule pamoja na moja kwa moja kwa wanafunzi wakiwa darasani.

Tanbihi :

Ifuatayo ni mifano ya taarifa muhimu ambayo inapaswa kuwekwa katika muktadha kwa ushirikiano na Wizara yenu ya Afya.

Ujumbe muhimu kwa walimu:

- Eneo hili kwa sasa linashuhudia kipindi cha joto kali.
- Joto kali linaweza kuwa hatari kwa maisha, na linaweza kuwa na athari hasi kwa uwezo wa wanafunzi kulenga masomo, na linaweza hata kuongeza matukio ya kutoelewana na mizozo. Ni muhimu kuhakikisha kwamba nyinyi na wanafunzi wenu mko salama wakati wa wimbi hili la joto.
- Hakikisha kuwa wanafunzi wenu wanakunywa maji ya kutosha. Wahimize kunywa maji mengi kabla ya kuhisi kiu.
- Dhukuru kufanya ushauri na kuahirisha matukio ya michezo hadi baada ya wimbi la joto.
- Dhukuru kuhamishia matukio ya michezo hadi vipindi vya baridi wakati wa mchana, kama vile mapema asubuhi.
- Iwapo jengo lenu lina kiyoyozi, dhukuru kuwa na vipindi vya mapumziko ndani ya nyumba. Iwapo jengo halina kiyoyozi, dhukuru kuwa na vipindi vya mapumziko au madarasa kwenye maeneo yenye kivuli, iwapo yana baridi zaidi ya joto la ndani ya jngo.
- Wanafunzi ni kiungo muhimu katika kuhakikisha kwamba wapendwa wao wako salama wakati wa wimbi la joto. Ili kusaidia ushauri huu muhimu kufika nyumbani, tafadhali sambaza taarifa muhimu zifuatazo kwa wanafunzi.


Ujumbe muhimu kwa wanafunzi:

- Eneo hili kwa sasa linashuhudia joto kali.
- Joto linaweza kuwa na madhara kwanu na kwa wapendwa wanu. Mjilinde na muwasaidie wengine kwa kusambaza taarifa ya kukabiliana na joto.
- Wakati wakati wa wimbi la joto, ni muhimu kuhakikisha mwili una maji ya kutosha kwa kunywa maji mengi, hata kabla ya kuhisi kiu.
- Wakati wa wimbi la joto, ni muhimu kwenu na kwa familia zenu kutumia muda wa angalau saa chache ndani ya siku katika eneo lenye baridi. Eneo hili linaweza kuwa majengo ya umma ambayo
- yana mfumo wa viyoyozi, bustani katika jiji lenu au maeneo mengine ya kujituliza ambaye yamefunguliwa kukabiliana na wimbi hili la joto. [WATU WALIOJITOLEA WAWEKE MIFANO NA MAENEO YALIYO KARIBU]
- Aidha, ni muhimu kuwajulia hali watu wa aila zenu pamoja na majirani walio na umri wa juu. Wahimize wazazi wenu kutafakari kuhusu watu wa umri wa juu ambao wanawajua. Waulize wazazi wako wawapigie simu au wawatembelee katika makazi yao kuwajulia hali.



KADI ZA HATUA 5: Brosha za ziara za shule

Kadi za hatua ni brosha ambayo inaweza kuchapishwa na kusambazwa kwa wanafunzi.





KADI ZA HATUA 6: Kutambua shinikizo la joto

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kuhusu namna ya kutambua dalili za shinikizo la joto.

Dalili za hatari ya kulemewa na joto:

- Kutokwa na jasho jingi kuliko kawaida
- Joto la kawaida au la chini
- Ngozi baridi, iliyokwajuka, yenye kunata
- Kuzirai au kizunguzungu
- Maumivu ya kichwa
- Mpigo wa kasi wa moyo au mpigo hafifu
- Maumivu ya misuli
- Kichefuchefu au kutapika

Dalili za hatari ya kiharusi

- Ngozi nyekundu, moto na iliyokauka (bila kutoa jasho)
- Mpigo wa kasi wa moyo
- Kupotewa na fahamu
- Kuwangwa na kichwa
- Tabia isiyo ya kawaida au dalili za kukanganyikiwa.
- Joto jingi mwilini

Kiharusi huhatarisha maisha-piga simu kuomba msaada wa matibabu ya dharura mara moja!



KADI ZA HATUA 7: Kutoa huduma za kwanza kwa waliolemewa na joto

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kuhusu huduma ya kwanza kwa waliolemewa na joto.


Huduma ya kwanza kwa waliolemewa na joto

- Mtoto aogeshwe maji baridi.** (Illustration: A man and a woman cooling a child in a blue tub.)
- Mweke mtu mahali patulivu, penye kiyoyozi, penye kivuli, iwapo inawezekana.** (Illustration: An air conditioner unit.)
- Mweke mtu huyo kwa njia ya kustarehesha apate kupumzika.** (Illustration: A person lying on the floor with a glass of water.)
- Mchunguze mtu huyo kwa makini kubaini maumivu yoyote yanayotokana na joto na umtulize mtu huyo hadi msaada ufike.** (Illustration: A person in a white coat and mask attending to a person on the floor.)
- Mfunike mtu huyo kwa kitambaa kilicholoa na utumie feni au ukungu ili kumtuliza.** (Illustration: A person in a white coat and mask attending to a person on the floor.)
- Iwapo mtu huyo angali na fahamu na hatapiki, Mpe maji anywe kidogo kidogo.** (Illustration: A person lying on the floor with a glass of water.)
- Tafuta ushauri wa daktari na ufuatilie maagizo yanayotolewa.** (Illustration: A hospital building, an ambulance, and a stethoscope.)
- Fanya ukaguzi kamili kwa kuchukua vipimo vya joto na kuchukua hatua za dharura zinazohitajika.** (Illustration: A clipboard, a first aid kit, and a thermometer.)



KADI ZA HATUA 8: Kutoa huduma za kwanza kwa walio na kiharusi

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kuhusu huduma ya kwanza kwa walio na kiharusi.



Piga simu kwa nambarai ya dharura ili kupata ambulensi mara moja.


Huduma ya kwanza kwa wenye kiharusi

Tekeleza hatua za kutuliza joto mara moja. Tumbukiza mwili wote (kuanzi shingo hadi chini) katika maji yenye joto la nyuzi 1-26°C (33.8-78.8°F) hadi joto la mwili wa mtu huyo ni chini ya nyuzi 39°C (102.2°F). Iwapo haiwezekani kumtumbika katika maji, tumia mbinu zifuatazo kutuliza joto:

Mpeleke mtu huyo kwenye mahalo patulivu penye kupitisha hewa.

Mtulize mtu huyo kwa kumrashia maji yenye joto la kawaida kwenye ngozi yake au kuipanguza ngozi kwa kitambaa baridi.

Tengeneza ujia wa upepo kwa kufunga shuka kando kando, wala sio juu, ya mwili wa mtu huyo. Tumia feni kuelekeza upepo baridi juu ya mwili wa mtu huyo.



Kutetemeka ni mchakato wa moja kwa moja wa misuli ambao huupasha mwili joto. Kutetemeka kutaongeza joto mwilini hata zaidi. Iwapo mtu ataanza kutetemeka, acha kumtuliza mara moja na umfunike hadi atakapoacha kutetemeka. Akishaacha kutetemeka, anza tena kuroa huduma ya kwanza.

Weka vibunda baridi au barafu iliyofungwa kwenye shingo, mapja na makwapa ya mtu huyo. Haya ni maeneo ambapo mishipa mikuu ya damu ipo karibu na ngozi, na hivyo ni njia ya haraka kabisa ya kusafirisha damu iliyotulizwa kwa baridi kote mwilini.

Mpe mmumunyo wa elektroliti. Huu unaweza kuundwa kwa kuongeza chumvi kidogo na sukari kidogo kwa glasi ya maji. Usimpe mtu huyo kinywaji chochote kupitia mdomoni iwapo mtu huyo hana fahamu kabisa.

Toa mavazi yasiyohitajika. Legeza nguo zilizobana.

Iwapo mtu huyo ana fahamu kabisa, mketishe chini ili umsaidie kunya na umpe kinywaji kilicho fufutende – sio baridi.



KADI ZA HATUA 9: Kuongea na wamiliki wa biashara

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo na ujumbe muhimu kuhusu namna ya kusema na wamiliki wa biashara na meneja wa biashara kuhusu hatari za joto kali na usalama wa wafanyakazi.

Ujumbe muhimu:

- Eneo hili kwa sasa linashuhudia joto kali.
- Joto kali linaweza kusababisha maafa, pia linaweza kuwa na athari hasi kwa biashara yenu. Ni kuhakikisha kwamba nyinyi na wanafunzi wenu mko salama wakati wa wimbi hili la joto.
- Mnaweza kubadilisha saa za kazi ili watu watumia muda mfupi nje wakati wa kipindi cha joto kali mchana. Kwa mfano, wasilisha bidhaa mapema asubuhi au jioni kabisa.
- Hakikisha wafanyakazi wanafikia maji ya kunywa wakati wote na uwahimize wanywe maji ya kutosha.
- Hakikisha ofisi, maduka na mahali pengine pa kazi pamedhibiti joto.
- Msiwe wagumu sana kwa saa za kazi kwa kuwa usafiri wa umma unaweza kuathiriwa na hali joto ya hewa.
- Wahimise wafanyakazi kuvaa mavazi yenye rangi inayong'aa, yasiyo mazito ili kutuliza joto. Dhukuru kutohimiza uvaaji wa tai na suti.
- Toa muda wa mapumziko mara kwa mara na mfumo tosha wa kuptitisha hewa safi kwa watu wa umri wa juu, mama wajawazito, watu walio na magonjwa ya kuselelea, na wengine walioorodheshwa kwenye *Kisanduku 2: Kutambua watu walio katika hatari ya kudhurika*.



KADI ZA HATUA 10: Usalama wa wafanyakazi wakati wa joto kali zaidi

Kadi hii ya hatua ni picha zenye taarifa kwa wafanyakazi kuhusu jinsi wanaweza kuzuia shinikizo la joto mahali pa kazi. Inaweza kuchapishwa na kusambazwa wa wafanyakazi wengine na meneja. Tolea la bango la kadi hii pia linapatikana.


5 Vidokezo vya kudumisha usalama wa wafanyakazi katika joto



1. Punguza kiwango cha kazi pole pole na uongeze muda wa mapumziko, hasa kwa wafanyakazi wa nje, wafanyakazi wapya na wale ambao hawajakuwa kazini kwa muda. Mpe kila mmoja muda wa kuzoea kufanya kazi katika hali za joto.

2. Badilisha mpangilio wa kazi na uweke vipindi vya mapumziko vya mara kwa mara, katika maeneo yenye maji na kivuli aumaeneo yenye kiyoyozi.

3. Hakikisha wafanyakazi wanapata maji baridi ya kutosha karibu na maeneo ya kazi.



4. Teua mtu wa kukagua hali zilivyo na kuwalinda wafanyakazi walio katika hatari ya shinikizo la joto.

5. Dhukuru kuvaa mavazi salama yanayosaidia kutuliza joto.



KADI ZA HATUA 11: Usalama wa watu waliojitolea

Kadi hii ya hatua inatoa mwongozo kwa watu waliojitolea kuhusu njia ya kuwa salama wakati wa shughuli za kuwafikia watu wakati wa mawimbi ya joto.

Ujumbe muhimu:

Usalama wako ni wa muhimu sana. Unapokuwa salama basi unaweza kuwasaidia wengine kuwa salama.

- Hakikisha unakunwa maji ya kutosha. Kunywa maji hata kabla ya kuhisi kiu.
- Iwapo unamulikwa moja kwa moja na joto, hakikisha uko na vipindi vya mapumziko vya mara kwa mara. Dhukuru kuvaa kofia pana kulinda uso, mafuta ya kukinga miale ya jua na mavazi yenye rangi inayong'aa, yasiyo mazito ili kuepuka kumulikwa moja kwa moja na jua na kutuliza joto.
- Katika baadhi ya maeneo, joto kali na unyevu huenda likaongeze idadi ya mbu. Iwapo hali hii inatokea ulipo, dhukuru kufukiza dawa ya kufukuza mbu.
- Punguza kipindi cha kazi kwa watu waliojitolea hasa wakati wa siku ambapo joto ni kali sana.
- Piga simu badala ya kufanya ziara inapowezekana.
- Tafuta jaketi nyepesi ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu ya au vaa nembo/kadi yenye jina wakati wa vipindi vya joto kali.
- Wajulie hali watu wengine waliojitolea ili kuihakikisha kwamba wako salama.
- Tambua dalili za ugonjwa unaohusishwa na joto kwako na kwa wenzako.

Chunguzi Maalum



UCHUNGUZI MAALUM 1: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Kenya

Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Kenya hushirikiana na wadau kutambua hatari zilizokithiri kutokana na joto katika mitaa ya mabanda jijini Nairobi.

KUELEWA MAENEO YANAYOTAMBULIWA KWA HATARI YA JOTO

Wakati wa msimu wa joto mnamo mwaka wa 2015/16, Jijini Nairobi, Kenya watafiti walichunguza mabadiliko ya viwango vya joto kote jijini kwa kujumuisha mbinu za upimaji kutoka mbali na mfumo wa muda wa vipima joto. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha uwepo wa visiwa vidogo vya joto katika maeneo ya mitaa ya mabanda jijini Nairobi. Hapa, joto aghalabu lilikuwa nyuzi kadhaa juu ya joto lililorekodiwa na kituo rasmi cha kutathmini joto jijini Nairobi kilichoko kwenye sehemu ya jiji yenye miti zaidi. Tofauti hii ya viwango vya joto pengine ilitokana na wingi na aina ya majengo katika mitaa hii pamoja na utovu wa maeneo yenye ,miti Aidha, inaambatana na tofauti za viwango vya joto iliyobainishwa katika tafiti nyingine kuwa na athari hasi kwa afya ya umma. Matokeo ya utafiti kutoka Nairobi yaliibua maswali muhimu kwa wanaosimamia huduma za dharura katika jiji hili, kama vile jinsi ya kujumuisha viwango vya juuvya joto vilivyopatikana kwenye mitaa ya mabanda katika kubuni mfumo wa kutoa ilani za mapema, na hivyo kutoa ilani katika sehemu za jiji ambapo joto sio kali sana ilikilinganishwa na sehemu nyinginezo za jiji.

Utafiti huu uliendeshwa kwa ushirikiano baina ya shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Kenya, Kituo cha kushughulikia Kubuni Mfumo wa utabiri wa tabianchi na Matumizi ya utabiri huu, Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Marekani, Kituo cha tabianchi cha Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu, Chuo Kikuu cha Johns Hopkins kule Baltimore, Maryland, Marekani na Taasisi ya kiufundi ya Blacksburg, Virginia, Marekani.

Mtu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Kenya aongea kuhusu hatari za moto katika mtaa wa Muku, jijini Nairobi. Mradi huu pia ulitathmini tofauti za viwango vya joto kote jijini.

Picha: Juozas Cernius/ Msalaba Mwekundu Marekani





UCHUNGUZI MAALUM 2: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam

Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Viet Nam, kwa msaada wa kiufundi kutoka kwa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Ujerumani, lilibuni mbinu za kubainisha athari likilenga kuchagua maeneo ya kutekeleza miradi katika Hanoi, Viet Nam.

KUBAINISHA ATHARI JINI HANOI ILI KUCHAGUA MAENEO YA UTEKELEZAJI

Idadi kubwa ya watu jijini Hanoi na tofauti katika ubora wa majengo na hali zilifanya vigumua kutambua wanaonufaika na ilani za hatua za mapema za kupunguza athari za mawimbi ya joto. Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam lilihitajika kujibu maswali yafuatayo: Tutawasaidia nani? Nani walio katika hatari kuu ya kudhurika? Ni maeneo yapi yenye joto kali zaidi jijini? Watu walio katika hatari kubwa ya kudhurika wanapatikana wapi?

Ili kupata majibu, Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam — kwa msaada wa kiufundi kutoka kwa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Ujerumani- lilibuni mbinu ya kubainisha iliyosaidia katika kuchagua watakaonufaika na maeneo ya mradi. Kifaa hiki cha kusaidia kufanya maamuzi ni mfumo wa kidijitali ambao unazalisha viwango vitatu vya taarifa (hatari ya kudhurika, mfichuo na hatari) ambayo inatumika kupata maeneo yenye uwezo wa kuwa na athari kubwa zaidi.

Watu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa wanasambaza maji wakati wa wimbi la joto mwaka wa 2015. Ramani ya maeneo yaliyo katika hatari ya kuathiriwa na Hatari ya joto jijini Hanoi.

Picha: Msalaba Mwekundu Ujerumani


Mfumo wa kidijitali ulisaidia shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam na Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ujerumani kuendesha utafiti wa jiji zima na kuibuka na ramani tatu zinazowakilisha hatari ya kudhurika, mfichuo na hatari kwenye wilaya zote 12 za wadi 168 za jiji la Hanoi. Safu hizo tatu za data zilikuwa ifuatavyo:

- **Hatari ya kudhurika:** hutambua na kuhesabu idadi ya watu walio katika hatari ya kudhurika (watoto chini ya umri wa miaka 5. Watu wa umri wa juu na watu wenye ulemavu).
- **Mfichuo:** hutambua na kuhesabu idadi kamili ya watu waoaishi kwenye mitaa ya mabanda na mitaa ya watu wa kipato cha chini ambapo hakuna viyoyozi.

- **Hatari:** Huonyesha msambao wa visiwa vya joto jijini Hanoi kutokana na taasisi ya utabiri wa hali ya hewa, haidrolojia na mabadiliko ya tabianchi.

Baada ya kuweka taarifa ya safu hizi tatu pamoja, ramani ya utabiri wa athari (pia huitwa ramani ya ulengaji) inaundwa na huonyesha wadi zilizo katika hatari kubwa zaidi ambapo mfichuo na hatari ya kudhurika huingiliana na hatari.

Mnamo 2019, maeneo yaliyo katika hatari kubwa zaidi jijini Hanoi yalikuwawilaya 12 za mjini na wadi 168 (zimeoneshwa kwa mipaka ya rangi ya kijani kibichi iliyokolea kwenye ramani kuelekea kushoto).





UCHUNGUZI MAALUM 3: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa

Kwa kushirikiana na mamlaka za mitaa, shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa hufuatilia hatari za joto kutoka misimu hadi majuma na siku ili kuwezesha mikakati ya kuokoa maisha.

KUTATHMINI NA KUKABILIANA NA ILANI ZA JOTO KWA USHIRIKIANO NA SERIKALI

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa hushirikiana na wenzao kutoka serikalini katika viwango vya mitaa, eneo na kitaifa ili kutathmini na kukabiliana na tukio la wimbi la joto. Kuna viwango vinne vya uwezesaji ambavyo hutathminiwa:

1. Tathmini ya msimu
2. Kutazamia na kujiandaa
3. Kuanzisha shughuli za kukabiliana na wimbi la joto.
4. Utafutaji wa kina wa rasilimali za dharura ili kukabiliana na wimbi kali la joto.

Mnamo 2019, nchi ya Ufaransa ilishuhudia mawimbi mawili ya joto. La kwanza lilidumu kwa siku tisaambapo zaidi wa watu 1,160 waliojitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa walitumiwa katika kusambaza maji, kusimamia maeneo ya kutuliza joto na kufanya ziara za nyumba hadi nyumba kuwajulia hali watu waliokuwa katika hatari ya kudhuruika. Watu wa kujitolea walitoa zaidi ya saa 34,000 za msaada ambazo ziliwasaidia watu 7,323. Serikali ya kitaifa kwa ushirikiano na serikali za mtaa na Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa kwa sasa wanadurusu mpango uliopo wa kukabiliana na wimbi la joto ili kujiandaa vyema zaidi kwa mwimbi ya joto ya mara kwa mara na makali zaidi kutokana na mabadiliko ya tabianchi katika siku zijazo.

Watu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Ufaransa wanasambaza maji wakati wa wimbi la joto mwaka wa 2015.
Picha: Croix-Rouge française -COM DT 75 -Benjamin Vancrayenest





UCHUNGUZI MAALUM 4: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi hushirikiana na wadau wa Mitaa na wa kitaifa kubuni mpango wa utendaji kukabiliana na joto nchini Uholanzi.

KUUNDA MPANGO WA UHOLANZI WA KUKABILI JOTO KWA USHIRIKIANO NA SERIKALI

Serikali ya Uholanzi iliunda mpango wa kukabiliana na joto mnamo 2007, baada ya msimu wa joto kali lililosababisha maafa mwaka wa 2006. Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi, Taasisi ya Uholanzi ya Afya ya umma na Mazingira pamoja na wadau wengine waliongoza undaji wa mpango huo. Lengo lao kuu lilikuwa kubainisha taratibu za kuwasilisha ujumbe wa kujiandaa kwa umma, uliotokana na utabiri wa hali ya hewa kutoka kwa Taasisi ta kifalme ya utabiri wa hali ya hewa nchini Uholanzi. Kuadamana na mchakato huu, Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi aidha liliunda mkakati wake wa mawasiliano uliolenga makundi mahususi yaliyo katika hatari kuu ya kudhurika.

Watu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi wanamjulia hali jirani wakati wa wimbi la joto mnamo 2018.

Picha:

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi

Tangu mchakato huu wa upangaji, Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi limeongoza shughuli mbalimbali zikiwemo ziara za nyumba hadi nyumba kwa watu wa umri wa juu ili kuhakikisha usalama wao na kusambaza ujumbe muhimu kuhusu kuwa salama wakati wa wimbi la joto. Shirika la Msalaba Mwekundu pia hutoa huduma za kwanza wakati wa matukio ya burudani na ya michezo. Isitoshe, Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi hutumia michezo kujenga ufahamu, kama vile 'Bloedhete Bingo' au 'Bloody Hot Bingo' ambayo ni njia ya kuburudisha ya kusambaza ujumbe a jinsi ya kuwa salama wakati wa wimbi la joto.



Kwa kutazama mbele, mnamo 2019, serikali ya Uholanzi ilianzisha mpano wa kutekeleza suluhu la kudumu katika ngazi za mitaa kupitia kwa hatua kama vile kuongeza bustani zenye miti na kuongeza maeneo yenye vivuli pamoja na Kuongeza idadi ya vituo vinavyotoa maji ya kunywa. Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uholanzi ni mdau muhimu katika majadiliano haya, hasa tukizingatia uwezo wake wa kuwasilisha shauku za jamii na tajriba zake katika kupunguza hatari za joto tangu 2006.



UCHUNGUZI MAALUM 5: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India

Mbinu ngeni za shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India za kusambaza ujumbe kuhusu hatari za joto jijini New Delhi.

MAKUNDI YA GHAFLA KUKABILIANA NA JOTO JIJINI NEW DELHI, INDIA

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India na Idara ya utabiri wa hali ya hewa nchini India zilianza kushirikiana kwa karibu katika kutabiri mawimbi ya joto mnamo 2017 ili kupunguza athari kwa watu walio katika hatari ya kudhurika.

Mnamo Juni 2017, vijana 15, wafanyakazi na watu wa kujitolea katika Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India walipata njia mpya ya kuwafahamisha watu jinsi ya kujiandaa kwa ajili ya wimbila joto lililokaribia: kundi la ghafla. Kundi la Ghafla ni miondoko inayofuata utaratibu ya nyinbo na densi, inayofanywa mahali hadharani bila kutangazwa, ili kuvuta nahdhari ya wapita njia; na, katika hali hii, kuwasilisha ujumbe muhimu.

Ujumbe ulikuwa sahili: kunywa maji mengi, funika kichwa chako, na “pumzika, pumzika, pumzika” baina ya saa sita na saa tisa- masaa yaliyokuwa na joto kali mdani ya siku.

Jumla ya makundi nane ya ghafla yalikutanika katika muda wa siku nne kwenye maeneo tofauti ya New Delhi. Watazamaji walikusanyika kadri washiriki katika makundi haya ya ghafla walivyocheza densi. Mamlaka ya Kusimamia Viwanja vya Ndege ya Delhi hata ilialika Shirika la Mwekundu kufanya makundi ya ghafla katika sehemu nne tofauti za uwanja wa kitaifa na wa kimataifa wa ndege ili kuwahamasisha wageni na wafanyakazi jinsi ya kukabiliana na viwango vya joto kutokana na wimbi la joto. Ujumbe ulipokelewa vyema na aghalabu ulirudiwa sisisi. Katika soko la Sarojini Nagar kusini mwa Delhi, wachuuzi, wanunuzi, wamiliki wa maduka na wapita njia waliacha shughuli zao kutazama kundi la ghafla.

Watu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini India wacheza wakati wa wimbi la joto mnamo 2017. Picha: Aditi Kapoor/Kituo cha Tabianchi





UCHUNGUZI MAALUM 6: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina hujenga ufahamu kuhusu hatari za joto kupitia kwa mitandao ya kijamii.

KUTUMIA MITANDAO YA KIJAMII KUSAMBAZA UFAHAMU KUHUSU KUJILIZA WAKATI WA JOTO

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina limetambua mitandao ya kijamii kama njia mojawapo faafu ya kuwafiklia watu. Kutokana na haya, imebuni nyenzo mbalimbali za taarifa na mafunzo ili kuongeza ufahamu wa jinsi ya kukabilaiana na wimbi la joto. Nyenzo hizi husambazwa kupitia Facebook, Instagram, Twitter na WhatsApp.

Matawi hutuma nyenzo hizi mara kwa mara, hasa kabla ya miezi ya joto msimu wa joto. Aidha, zinatolewa na Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina pindi tu tahadhari ya siku zenye joto kali inapopokelewa kutoka kwa idara ya kitaifa ya utabiri wa hali ya hewa.

Wateja wametambua umuhimu wa nyenzo hizi pamoja na wepesi wa kuzifikia kupitia mitandao ya kijamii. Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Argentina kwa sasa linajadiliana na serikali ya Buenos Aires kuhusu kubuni mpango kabambe wa hatua za kukabili joto katika jiji hilo.



UCHUNGUZI MAALUM 7: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Australia

Huduma ya Telecross REDi ambapo watu wanaojitola kutoka kwa shirika la Msalaba Mwekundu nchini Australia huwapigia simu watu waliokwisha sajiliwa kila siku kuwajulia hali wakati wa mawimbi ya joto.

HUDUMA YA SIMU KWA WAKAAZI

Huduma ya Telecross REDi huwasaidia watu kwa kuwapigia simu kila siku wakati wa mawimbi ya joto yaliyotangazwa. Huwezesha na Idara ya Huduma za Binadamu ya Australia ya Kusini wakati hali ya tukio kali la hewa inatangazwa. Watu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Australia huwapigia simu wateja waliosajiliwa tayari ili kuwajulia hali. Wanaopiga simu huwauliza watu jinsi wanavyoendelea na kuwakumbusha hatua muhimu zitakazowasaidia kukabiliana na matukio makali ya hali ya hewa. Iwapo simu haitajibiwa au iwapo mtu yumo katika hatari, mchakato wa dharura huwezesha ili kuhakikisha usalama na ustawi wa mteja husika. Watu katika jamii ambao wamo katika hatari wakati wa matukio makali ya hali ya hewa na wanahitaji msaada kupitia kwa njia ya simu wakati huu huhimizwa kujisakili kwa huduma hii. Hii inajumuisha watu waoaishi peke yao, walio na ulemavu, walio na matatizo ya kiakili, wamezuiwa kutoka ndani ya nyumba, dhaifu, wazee, wanaopata nafuu kutokana na ugonjwa au ajali, au walio na magonjwa ya kuselelea kama vile kisukari au ugonjwa wa moyo. Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea Telecross REDi [webpage](#).

Mtu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Australia anawapigia simu watu walio katika hatari ya kudhurika wakati wa wimbi la joto.

Picha: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Australia





UCHUNGUZI MAALUM 8: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania hutoa taarifa muhimu kwa watu walio katika hatari kupitia kwa kampeni za ujumbe kwa njia ya simu.

Mtu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania akiwapigia simu watu walio katika hatari ya kudhurika wakati wa wimbi la joto.

Picha: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania

KAMPENI ZA UJUMBE KUPITIA KWA SIMU

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania huwa na kampeni za ujumbe kupitia kwa simu kila mwaka kuanzia mwezi Juni hadi Septemba katika mikoa ambapo kwa kawaida joto huwa kali sana msimu wa joto. Kampeni hii huwalenga wale wanaojulikana kuwa katika hatari ya kudhurika na joto kali, kampeni hulenga kutathmini afya ya wateja na kutoa ushauri ambao utawasaidia kukabiliana na joto kali.

Kwa kawaida, opareta hupiga hadi simu tatu, akiuliza maswali ya utafiti na kutoa ushauri faafu kwa kila mmoja. Kwa mfano, opareta anaweza kuuliza: “Je, wewe hunywa viowevu kiasi gani ndani ya siku moja wakati wa msimu wa joto? (Hivi vinapaswa kuwa maji, maji asilia ya matunda au vinywaji vingine visivyo na kafeini, sukari au vileo.)”. Opareta anaweza kuwapa taarifa kama vile:

“Tunapaswa kunywa angalau lita 1.5 ya maji kila siku ili kuwa na afya njema, Hata kama hatuhisi kiu au kuhisi joto.”. Kisha anaweza kufanya mapendekezo, kama vile: “Hakikisha unabeba chupa ndogo ya maji kila wakati unapokuwa nje na uyanywe polepole. Jaribu unywe glasi moja ya maji kila baada ya saa mbili, ukitumia saa au njia nyingine kukukumbusha.”

Simu hizo tatu huwa zimeratibiwa kiotomatiki, huku simu kuhusu wimbi la joto zikipigwa kila baada ya siku 15. Opareta daima hufuata maswali sawa ya kiutafiti, lakini hahitajiki kuuliza yale yaliyojibiwa tayari kwa mwitikio wa ndiyo hapo awali.





UCHUNGUZI MAALUM 9: Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong

Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong hutoa programu za mafunzo kwa shule ili kuimarisha ufahamu kuhusu hatari za joto na kupanua usambazaji wa taarifa kwa jamii pana zaidi.

KUIMARISHA UWEZO WA JAMII KUKABILIA MAWIMBI YA JOTO

Mnamo 2017, Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong, tawi la Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Uchina, liliunda mpango wa kimkakati wa miaka mitano wa kuimarisha uwezo wa jamii. Joto lilitambuliwa kuwa hatari inayoibuka kutokana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kujumuishwa ndani ya mkakati huo.

Baada ya kutambua watoto na watu wa umri wa juu kuwa walio katika hatari kuu ya kudhurika wakati wa wimbi la joto, mnamo 2018 shirika la Msalaba mwekundu la Hong Kong lilianzisha mpango wa kutoa mafunzo kwa watoto wa shule, ikiwemo wale wa chekechea na shule za msingi na sekondari. Mpango huu ulijumuisha Seti Mpya ya Kytoa Mfunzo Jumuishi ya Kujiandaa kwa Ajili ya Majanga, ilianguzia mada kama vile mabadiliko ya tabianchi, mawimbi ya joto, matukio ya baridi, moto katika majengo, magonjwa yanayosambazwa, na huduma ya kwanza ya kimsingi.

Wafanyakazi na watu wa kujitolea sabibi na saba walipewa mafunzo kama wataalamu wa kutoa mafunzo na wakaanza kutoa mafunzo hayo mnamo Mechi 2019. Wanafunzi walifundishwa kuhusu dhana ya mabadiliko ya tabianchi na mawimbi ya joto na kupewa vidokezo vya kupunguza athari zake. Walihimizwa kuhifadhi umeme na kulinda mazingira ili kupunguza visababishi vya mawimbi ya joto. Mnamo 2019, zaidi ya wanafunzi 2,600 kutoka shule 13 walipewa mafunzo.

Kwa wakati huo huo, Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong lilianzisha mpango wa tathmini za nyumbani kwa watu wa umri wa juu, kutathmini ufikiaji wa umeme na vifaa vya kutuliza joto. Nyumba zilizokuwa na uhitaji zilipewa feni za umeme, hasa zilizogawika katika nyumba za kukodi au sehemu ndogo ndani ya jengo kubwa la makazi.

Mpango wa utoaji mafunzo kwa shule Pia ulisambazwa kwa jamii ili kuimarisha ufahamu wa athari za Mabadiliko ya tabianchi, na kuimarisha uwezo wa watu kukabiliana na majanga. Ufahamu wao uliimarishwa na mwitikio umekuwa chanya. Kwa sasa watu wako radhi kushiriki katika shughuli ithibati kwamba mahusiano ni njia mojawapo ambayo ni faafu zaidi Katika kuimarisha uwezo wa jamii.

Mtu wa kujitolea kwa ShShirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong atembea na mtu wa umri wa juu katika jamii wakati wa kuwajulia hali.
Picha: Shirika la Msalaba Mwekundu la Hong Kong





UCHUNGUZI MAALUM 10: Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan

Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan huwezesha maeneo ya kusambaza maji ya kunywa kulingana na utabiri.

KUWEZESHA USAMBAZAJI WA MAJI YA KUNYWA KUTOKANA NA UTABIRI

Mnamo Julai 10 mwaka wa 2019, kulitolewa tahadhari ya wimbi la joto la siku 7 (Julai 12-18, 2019) na Idara ya utabiri wa hewa ya Tajikistan (National Hydrometeorological Service of the Republic of Tajikistan) ikilenga sehemu za kusini, kaskazini na kati za nchi, ambapo viwango vya joto vilitabiriwa kupanda kufikia hadi nyuzi 44-46°C. Tahgadabri hii iliongezwa mara mbili -hadi Agosti 10, 2019. Kutokana na hali hii, Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan (RCST) lilifungua vituo vya kusambaza maji ya kunywa, kwa ushirikiano wa karibu na Kamati ya Tajikistan ya Matukio ya Dharura na Ulinzi wa Wananchi pamoja na mamlaka ya mitaa.

Ufikiaji wa maji ni mojawapo wa tatizo kuu kwa watu wakati wa mawimbi ya joto nchini Tajikistan, hivyo basi usambazaji wa maji ni jamo la msingi. Kwa kushirikiana na mamlaka za serikali, RCST ilisambaza maji ya kunywa ya kila siku kwa vijiji vya Orzu, katika wilaya ya Zafarobod kwa watu waliokuwa katika hatari ya kudhurika waliokuwa wameathiriwa pakubwa na wimbi la joto. Kufuatia uchanganuzi wa kina wa nchi nzima, eneo hili lilibainishwa kuwa mojawapo wa maeneo yaliyo katika hatari kuu ya kudhurika na mawimbi ya joto. Kutokana na hya, nyumba 180 (watu 900) walipokea lita 13,500 za maji kila siku kwa kiwango cha lita 15 kwa kila mtu kila siku kwa mujibu wa viwango vya ubinadamu (SPHERE) kwa nyumba kutumia kunywa

na kudumisha usafi nyumbani. Kufikia Agosti 8, 2019, lita 391,500 za maji zilikuwa zimesambazwa ndani ya kipindi cha siku 29.

Kuambatana na mkakati wa mawasiliano wa RCST, kampeni za taarifa ziliendeshwa kwa jamii zilizolengwa na hospitali pamoja na kwenye maeneo ya umma. Shughuli hizi zilijumuisha taarifa kuhusu namna ya kupunguza hatari ya kiharusi.

Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan linasambaza maji ya kunywa wakati wa wimbi la joto mnamo 2019.

Picha kwa hisani ya:

Shirika la Hilali Nyekundu nchini Tajikistan





UCHUNGUZI MAALUM 11 : Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam

Wakati wa wimbi la joto mnamo Agosti 2019 Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam lilifungua vituo vya kutuliza joto na mabasi ya kutuliza joto ili kuwasaidia wakaazi wa Hanoi, nchini Viet nam kukabiliana na joto kali.

KUFUNGUA VITUO VYA KUTULIZA JOTO KUTEGEMEA UTABIRI

Wakati wimbi la joto lilitokea Hanoi baina ya tAgosti 11-14, 2019, Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Na, kwa msaada kutoka kwa Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Ujerumani, lilifungua vito vinne vya kutuliza joto vya jamii na kutoa mabasi matatu yaliyokuwa na mfumo wa kutuliza hewa ili kutoa mahali pemnye hewa baridi kwa watu waliokuwa katika hatari ya kudhurika. Mbasi ya kutuliza joto yalisafiri kwenye barabara za Hanoi, yakisambaza ujumbe wa kuwahamasisha watu na kusimama katika maeneo maalum ili kuwafikia wachuuzi reja reja na waendeshaji wa pikipiki. Watu wa kujitolea walipewa mafunzo ya kutoa huduma ya kwanza ya dharura ili kuwasaidia watu waliokuwa na dalili za shinikizo la joto.

Vituo na mabasi yalipokea watu 1,787 ndani ya siku nne ambazo vituo na mabasi yalikuwa wazi. Miongoni wa waliozuru vuto na mabasi, asilimia 24 ilikuwa wachuuzi reja reja, asilimia 23 ilikuwa waendeshaji pikipiki na asilimia 15 ilikuwa wafanyakazi za sulubu. Kwa wastani, vituo vilikuwa na joto la chini hadi nyuzi 7°C ikilinganishwa na joto la nje. Wachuuzi reja reja walikuwa kikundi kikubwa kilichokuwa na ziara za mara kwa mara, huku asilimia 60 wakizuru zaidi ya mara moja. Wageni walizuru vituo ili kuepuka, kupunguza au kupata nafuu kutokana na dalili zinazohusishwa na shinikizo la joto, huku wakidhihirisha uwezo wa kutambua dalili pamoja na radhi yao kuzichukulia hatua. Vituo vya kutuliza joto vilipokelewa vyema, huku asilimia 95 ya waliozuru wakieleza athari ya vituo hivi kama “chanya” au “chanya sana”.

Kuongea na wachuuzi reja reja kuhusu hatari zinazohusiana na joto kali.

Picha: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Viet Nam





UCHUNGUZI MAALUM 12: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania hufanya kazi ili kupunguza ajali za kufa maji wakati wa mawimbi ya joto.

KUHAKIKISHA WAKAAZI WAKO SALAMA WANAPOZURU UFUO

Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania hutoa usalama kwa wakaazi wakati wa miezi ya msimu wa joto, ambao aghalabu huanzia Juni wakati ambapo watu hufurika ufuoni kufurahia joto la msimu wa joto na kutuliza joto baharini. Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania linawajibikia asilimia 40 ya huduma za kuzuia kufa maji kwenye ufuo na kuliko maji ndani ya nchi (k.v. Maziwa, mito n.k.) kote nchini. Aidha, huwa linatoa huduma kama vile za huduma za haraka wakati wa dharura, ambulensi, boti za uopoaji na viti vya kiamfibia kwa walemavu.

Mtu wa kujitolea kwa Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania akizungumza na watu waliozuru ufuo wakati wa wimbi la joto. Picha: Shirika la Msalaba Mwekundu Nchini Uhispania

Kwenye ufuo, watu wa kujitolea kwa Msalaba Mwekundu na wafanyakazi huongea na watu waliozuru ufuo na kutoa vijikaratasi vinavyoeleza jinsi ya kuwa salama kwenye ufuo na kuepuka hatari, kama vile kuelemeza na joto na kiharusi, kuungua ngozi, kung'atwa na viwavi na kufa maji. Hii inajumuisha mafunzo ufuoni kuhusu maana ya mfumo wa bendera yenye rangi ambao hutoa taarifa kwa waogeleaji kuhusu iwapo ni salama kuingia majini au la.



Maandishi

Mwongozo huu uliandikwa na

Julie Arrighi^{1,2}, Roop Singh¹, Ramiz Khan¹, Bettina Koelle¹ na Eddie Jjemba¹.

Waandishi wangependa kuwashukuru wafuatao kwa kuandika baadhi ya visanduku, chunguzi maalum au karatasi za mwongozo katika mwongozo huu:

Nancy Claxton³ – *Kisanduku 3: Kuwahimiza na kuwadumisha watu waliojitolea*

Alison Freebairn³ – *Kadi za Kutenda 1: Mfano wa Tangazo la vyombo vya habari*

Jerome Faucet⁴ – *Uchunguzi Maalum 2: Ubainishaji wa athari jijini Hanoi, Vuet Nam ili kuchagua maeneo ya utekelezajina Uchunguzi Maalum 12: Kufungua vituo vya kutuliza joto kutegemea utabiri uliotolewa*

Aditi Kapoor^{1,3} – *Uchunguzi Maalum 5: Makundi ya ghafla ya kukabiliana na joto jijini New Delhi, India*

¹ Vituo vya Tabianchi vya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

² Kituo cha Kujiandaa kwa ajili ya Majanga Ulimwenguni.

³ Muungano wa Kimataifa wa Mashirika la Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

⁴ Shirika la Msalaba Mwekundu nchini Ujerumani.

Namna ya kuandika marejeleo ya mwongozo huu:

Arrighi, J., Singh, R., Khan, R., Koelle, B., Jjemba, E., *Mwongozo wa jiji kuhusu mawimbi ya joto Kwa matawi ya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu*. 2020.

Vituo vya Tabianchi vya Msalaba Mwekundu na Hilali Nyekundu

Waandishi pia wangependa kuwashukuru watu wafuatao (kwa kuzingatia mpangilio wa kialfabeti) kwa muda wao mwingi wa kusanifu mwelekeo wa mwongozo huu na kukaguayaliyomo:

Mariano Alfonsi, Croix-Rouge argentine ; Andrea Ando, Croix-Rouge italienne ; Shirley Blackshaw González, Croix-Rouge du Costa Rica ; Yvonne Breedijk, Croix-Rouge néerlandaise ; Noemie Brocas, Croix-Rouge française ; Fernel Campher, Croix-Rouge sud-africaine ; Pascal Cassan, Centre mondial de référence des premiers secours ; Nancy Claxton, Fédération internationale des sociétés de la Croix-Rouge et du Croissant-Rouge ; Erin Coughlan de Perez, Centre climatique ; Sandrine Dacunha, Croix-Rouge espagnole ; Raimond Duijsens, Croix-Rouge néerlandaise ; Knud Falk, Centre climatique ; Jerome Faucet, Croix-Rouge allemande ; Wolfgang Friedrich, Croix-Rouge allemande ; Bonnie Haskell, Centre mondial de préparation aux catastrophes ; Noor Jaber, Croix-Rouge libanaise ; Catalina Jamie, Centre climatique ; Eddie Jjemba, Centre climatique ; Hunter Jones, Global Heat Health Information Network ; Aynur Kadhihasanoglu, Fédération internationale des sociétés de la Croix-Rouge et du Croissant-Rouge ; Aditi Kapoor, Centre climatique ; Rachel Kirvan, Croix-Rouge britannique ; Irene Lui, Croix-Rouge de Hong Kong ; Sarafroz Mavlyanov, Société du Croissant-Rouge du Tadjikistan ; Grace Mawalla, Société de la Croix-Rouge de Tanzanie ; Fleur Monasso, Centre climatique ; Daniel Mutinda, Société de la Croix-Rouge du Kenya ; Ian O'Donnell, Fédération internationale des sociétés de la Croix-Rouge et du Croissant-Rouge ; Monica Owens Doyle, Croix-Rouge américaine ; Richard Smejkal, Croix-Rouge tchèque ; Habiba Sultana Shompa, Croissant-Rouge du Bangladesh ; Y oshiteru Tsuji, Croix-Rouge japonaise ; Ayub Twaha, Croix-Rouge ougandaise ; Ana Villa Mariquina, Croix-Rouge des Philippines ; Nicola Ward, Centre climatique ; Gavin White, Croix-Rouge américaine

Nakala hii ya mwongozo ilihaririwa na Sarah Tempest.

Ilisanifiwa na Eszter Sarody.

Michoro ilibuniwa na Jorge Martin.

Picha zenye taarifa zilibuniwa na Andrej Hribernik.

Maandalizi ya mwongozo huu yalifadhiliwa na Climate-KIC na yamepokea ufadhili kutoka kwa European Institute of Innovation and Technology, asasi chini ya Muungano wa Ulaya, chini ya mpango wa Horizon 2020, EU Framework Programme for Research and Innovation. Kituo cha Global Disaster Preparedness Center kilitoa rasilimali za ziada katika kuandaa mwongozo huu.

